Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 178 | RABIUL I/RABIUL II 1435 AH | FEBRUARY 2014 | TABLIGH 1393 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, Mwogopeni Mwenyezi Mungu na semeni usemi uliosawa. Atawatengenezeeni vizuri mwenendo wenu na Atawasameheni madhambi yenu; na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa. (Al Ahzab 33:71-72).

Khalifa Mtukufu awaambia Waahmadiyya:

Mtaheshimika kwa matendo sio maneno

Na Mwandishi wetu

Tokea hotuba iliyopita, yamekuwa yakiongelewa mambo yahusikanayo na marekebisho ya vitendo au Tarbiyyat (malezi), kwa masheikh, na kujumuisha wote wale waliojitoa wakfu, maamiri na wenye vyeo ndani ya Jumuiya, kwamba ni namna gani wanapaswa kutekeleza majukumu yao katika kujidhibiti na sababu zile zinazohujumu mrekebiko wa matendo, na ni mahitajio yepi ambayo wabashiri na viongozi wengine wa Jumuiya wanapaswa kuyatekeleza katika maisha yao na kuwaambiyayo wanajumuiya.

Hapa pia nifafanue kwamba, wale wanazuoni na wahubiri waliokuwepo katika zama za Hadhrat Muslihul Mauud r.a., miongoni mwao walikuwemo pia masahaba wa Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. na pia walikuwemo wale waliopata malezi toka kwa Masahaba r.a. Uhusiano wao na Allah na viwango vyao vya imani kwa hakika vilikuwa vya juu sana. Mapungufu yao hayakuwemo katika mambo haya.

Upungufu uliokuwepo, ambao Hadhrat Muslih Mauud r.a. aliuelezea, ni kwamba kulikuwa na haja ya kubadili vipaumbele, au kama vile mkazo ulivyokuwa ukitiliwa katika masuala ya kiitikadi, vivyo hivyo kulitakiwa kuwepo na marekebisho na malezi kwa watu, kwenye mambo ya kimatendo pia, kama vile ishara za Hadhrat Masih Aliyeahidiwa a.s., mahusiano yao binafsi na Mwenyezi Mungu, utii kwa ukhalifa na kuiheshimu nidhamu.

Lakini leo tunaona kwamba hatuna viwango vile katika mambo haya. Hivyo pana umuhimu hasa, pale nisemapo kwamba wabashiri na viongozi wa Jumuiya wajipime halafu ndio wawaeleze wanajumuiya. Yaani neno la kujipima, kutafakari na kutenda na kuonyesha mfano ni muhimu sana. Hapo ndipo maneno ya urekebishaji yatakapokuwa katika rangi ya ukweli.

Katika hotuba iliyopita ilitajwa namna ya kuongeza nguvu ya dhamira na kuondoa udhaifu wa kielimu. Lakini jambo la tatu katika suala hili, yaani njia ya kuondoa udhaifu katika utekelezaji wa mambo au namna ya kuongeza vipawa vya utekelezaji wa mambo. Leo nitasema kuhusiana na haya.

Kwa ajili yake, kama ilivyokwisha elezwa ndani ya hotuba zilizopita, tiba au msaada wa nje wahitajika, au yaweza kusemwa kwahitajika msaada

Endelea uk. 3

Ansarullah UK watafuta radhi za Mola wao

Wazidisha misaada ya Maji nchini

Na Pazi Mazongera

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania, chini ya ufadhili wa *Ansarullah* (Taasisi ya wazee wa Kiahmadiyya) Uingereza, imeendelea kuongeza misaada ya maji safi na salama nchini kwa kuongeza uchimbaji na ukarabati wa visima vya pamp za mikono.

Ili kufanikisha zoezi hilo, Ansarullah UK imemleta mtaalamu wake Mzee Saeed Lone kwa ajili ya kusimamia miradi hiyo. Tayari taasisi hiyo imeshachimba visima vya maji katika maeneo ya mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma Singida na Mbeya. Hivi karibuni msaada wa uchimbaji wa kisima cha maji safi unatarajiwa kutolewa huko Zanzibar.

Mbali na uchimbaji wa visima vipya shirika hilo pia limekuwa likisaidia masuala kadhaa yahusuyo maji kama vile matenki ya kuhifadhia maji. Miongoni mwa maeneo yaliyopata msaada huo ni shule ya sekondari ya Muhoro ambapo msaada huo ulipokelewa na Waziri wa afya na Ustawi wa Jamii Mh. Dr. Seif Rashid Suleiman katika viunga vya Masjid Salaam jijini Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri ambaye aliambatana na viongozi kadhaa waandamizi wa Wilaya ya Rufiji alipokelewa na Amir wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaundhry pamoja na viongozi wengine wa Jamaat.

Akimkaribisha Mheshimiwa Waziri, Amir Jamaat alimueleza mgeni kuwa Majlis Ansarullah ni taasisi iliyo chini ya Jumuiya ambayo ipo Uingereza imekuwa ikijitolea kupunguza matatizo na shida za maji katika maeneo mbalimbali hapa nchini na kumueleza kuwa matenki haya ni sehemu ya msaada huo kwa shule ya sekondari Muhoro. Akielezea furaha yake juu ya msaada huo, Mheshimiwa Waziri alisema kuwa kwa kweli msaada huo umekuja katika kipindi muhimu hasa ikizingatiwa kuwa Shule hiyo ilikuwa kwenye matatizo makubwa ya maji na ni msaada uliokuwa ukingojewa hasa na kuishukuru Jamaat na kuiomba kuendelea kusaidia katika maeneo mengine pia. Mheshimiwa



Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mheshimiwa Dr. Seif Rashid Suleiman (mwenye suti nyeusi) akipokea msaada wa matenki ya kuhifadhia maji safi kwa ajili ya shule ya Sekondari Muhoro ya Wilaya ya Rufiji. Anayesalimiana naye ni mwakilishi wa Ansarullah UK. Mzee Saeed Lone. Katikati yao ni Amir na Mbashiri Mkuu nchini Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry.

Waziri pia alitumia fursa hiyo kuwatambua viongozi wengine waliomlaki na kusalimiana nao. Aidha Taasisi hiyo ya Ansarullah ya Uingereza ilifanya ukaguzi wa miradi hiyo kupitia mjumbe wake Bwana Akram Ahmad ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha wasanifu majengo na wahandisi wa Kiahmadiyya duniani na kutembelea maeneo ya Mkongo, Ikwiriri, Kibiti na Bungu na kuridhishwa kwake na jinsi Jamaat Ahmadiyya Tanzania ilivyosimamia vizuri miradi hiyo ya maji.

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

UTAKASAJIWA NAFSI

Hapana shaka toka Jumuiya ya Waislamu Waahamdiyya ianzishwe mwaka 1889 kwa idhini ya Allah na mtoto wa kiroho wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Seyidna Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. imefanya kazi inayostahili heshima kwa kueneza mafundisho sahihi ya Islam, kufuta masingizio yote kuhusu Islam, kuonesha ubora wa mafundisho ya Islam, kulinganisha mafunzo ya Islam na dini nyingine ulimwenguni. Sasa dunia imepambazukiwa na alfajiri ing'arishayo.

Mng'arisho unaoonesha ya kwamba kitabu pekee ambacho ni *Laa Raiba Fiihi* kisicho na shaka ndani yakeni Quran Tukufu. Hakuna shaka ndani ya Kuruani tukufu. Hiki ni kitabu ambacho hata nukta moja haikupotea wala haitapokea kwani kimepewa ahadi – sisi ndio tulioteremsha mawaidha na sisi ndio tutakaoilinda. Kila silabi katika kitabu hiki iko vile vile bila kuguswa na mkono wa aina yoyote. Ni Qurani tukufu ile ile aliyoshushiwa mtukufu Mtume Mtukufu Muhamamd s.a.w. sheria 700 zilizomo katika Quran tukufu ndio njia inayomuwezesha binadamu kufikia shabaha ya kuumbwa kwake. Ahamdiyya imeondoa uchafu na tandabui vilivyokuwa vimezingira nyumba hii ya Islam. Na ikaeleza ya kwamba kila watu wamepata Mtume na wote wametoka kwa Allah na wote wanastahili heshima – njia bora ya kuondoa migogoro dunaini.

Kwamba Unabii ni neema na hivyo manabii wataendelea kuja ila unabii wa kuleta sheria mlango wake umefungwa. Nabii Issa kama walivyo manabii wote amefariki na wala hatorudi duniani. Binadamu anatakiwa atimize wajibu wake kwa Allah na kwa viumbe wa Allah.

Kwa kiwango kikubwa kazi hiyo imefanyika kwa ufanisi mkubwa na ushahidi ni msaada mkubwa ambao Jumuiya inaendelea kupata. Imesambaza vitabu, ujengaji wa misikiti na kwa msaada wa Mwenyezi Mungu tayari zipo tafsiri ---- za Quran tukufu katika lugha mbalimbali.
MTA inafanya kazi ya kueneza Islam duniani kote kwa saa ishirini na nne kila siku.
Hivi leo hakuna sheikh anayeweza kudiriki kuingia pambano na mtoto mdogo wa Kiahamadiyya kihoja. Alhamdulillah kazi hiyo imefanywa vizuri. Lakini kazi ya pili ya Masihi Aliyeahidiwa ilikuwa ni ujengaji wa khulka, kusafisha nafsi. Hii ni kazi ambayo Khalifa wa Tano Hazrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. ametupa Waahmadiyya kushughulika nayo. Kusafisha nafsi zetu. Kufanya kazi hiyo kw amapenzi na heshima huku tukielewa ya kuwa kama sisi hatumuoni Mweneyzi Mungu lakini Mwenyezi Mungu anatuona sisi na kila penye wawili basi wa tatu ni Mwenyezi Mungu. Kazi tuliyonayo ni kuziweka kwa vitendo amri 700 zilizomo katika Qur'an tukufu kwa vitendo. Na lazima tusahau kabisa fikra ya kwamba kuna makosa makubwa na kuna makosa madogo, kuna dhambi ndogo na dhambi kubwa. Alichokikataza Mwenyezi Mungu lazima kiachwe bila kugeuka na kungeuka.

Usafishaji wa nafsi unahitaji msaada mkubwa wa Mwenyezi Mungu. Tunaishi katika wakati mgumu sana. Tumezungukwa na miba na hivyo tunatakiwa tutembee kwa tahadhari kubwa. Na mshairi wetu Al-Ustaadh Khamis Sultan Wamwera hakukosea alipoimba.

Malfudhaat Sayedna Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Nasaha ihusuyo Taqwa

Syedna Ahmad as anasema, kwa kuitakia Jumuiya yangu kila la kheri inaonekana ni muhimu sana itolewe nasaha kuhusu taqwa yaani uchaMungu, kwani jambo hili ni wazi kwa mtu mwenye akili ya kwamba Mwenyezi Mungu Haridhiki kutoka jambo lolote isipokuwa kwa taqwa.
Mwenyezi Mungu Anasema, kwa hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wale wanaomcha, na wale wafanyao wema. AN-NAHL 129.
Jumuiya yetu haswa inahitaji uchaMungu kwa sababu wao wanahusika na mtu na wamo katika baiti yake ambaye amedai kuwa *maamur* (mtu aliyeamrishwa na Allah) ili watu kama hao waliokuwa wakijitumbukiza kwenye ubaguzi, uadui na ushirikina wa aina yoyote au walikuwa wakiipenda dunia kwa kiasi gani waokolewe kutoka mabalaa hayo yote.
Nyinyi mnaelewa ya kuwa akiugua mtu fulani, maradhi yake yawe madogo au makubwa kama yasifanyiwe tiba, mgonjwa hawezi kupona. Alama nyeusi ikitoka usoni mwa mtu inasababisha ahuzunike sana kwa kutafakari ya kuwa isije alama hiyo ikaanza kuongezeka na kuufanya uso wote kuwa mweusi vivyo hivyo kunakuwa na alama moja ya uasi moyoni. Maasi madogo kwa sababu ya uvivu yanakuwa makubwa, madhambi madogo ni alama ile ile ndogo ambayo ikiongezeka mwishowe inaufanya uso wote kuwa mweusi.
Mwenyezi Mungu ni Karimu Mwenye rehema na pia ni Kahari na Mwenye kulipiza kisasi, Anaona jumuiya ya watu ambao madai yao na maneno yao ni mengi lakini hali ya matendo hailingani nayo, basi hasira na ghadhabu yake huwa inaongezeka kisha kwa kuiadhibu jumuiya kama hiyo Anawateua makafiri. Wale ambao wana elimu ya historia wanajua vizuri ya kuwa mara nyingi waislamu waliuawa kwa kupitia makafiri kama vile Changez Khan na Halaku Khan waliwaangamiza Waislamu ingawaje Mwenyezi Mungu Aliwaahidi waislamu kuwahami na kuwasaidia lakini tena waislamu wakashindwa. Matukio yaaina hiyo yalijitokeza katika nyakati tofauti, sababu yake ndiyo hii ya kuwa wakati Mwenyezi Mungu Anapoona ya kwamba dai la kusema LAA ILAHA ILLALLAH lipo lakini moyo wake waelekea upande mwingine na kutokana na matendo yake imeangukia dunia tu basi sifa yake ya kahari inaonesha rangi yake.

Ulinganifu baina ya usemi na matendo

Hofu ya Allah Taala imo ndani yake ya kuwa binadamu achunguze vizuri ya kwamba kauli na matendo yake zinalingana kwa kiasi gani, kisha akigundua ya kuwa matendo yake hayalingani na usemi wake basi aelewe ya kuwa atapata ghadhabu ya Mungu. Moyo usiotakasika hauwezi kuthaminiwa mbele ya Mwenyezi Mungu lau kama kauli iwe imetakasika kiasi gani, bali utamchukiza Mwenyezi Mungu zaidi.
Basi Jumuiya yangu ielewe ya kuwa wamekuja kwangu kwa lengo la kupandiwa mbegu za kiroho ili wawe kama miti yenye kutoa matunda, basi kila mmoja ajichunguze nafsini mwake ya kuwa undani wake ukoje? Kama Mungu Apishe mbali jumuiya yangu pia ina hali hii yakuwa juu ya ulimi kuna jambo moja ilhali moyoni lipo jingine basi mwisho wake hautakuwa na heri. Mwenyezi Mungu Anapotazama ya kuwa kuna jumuiya ambayo inadai kwa maneno tu na upande mwingine moyoni hamna kitu chochote basi Yeye ni Mkwasi, Naye pia Haijali. Bishara ihusuyo ushindi wa vita ya Badri ilikuwa imekwishatolewa tayari na kulikuwa na matarajio yote ya kupata ushindi lakini bado Mtume Mtukufu saw alikuwa akiomba sana maombi kwa kulia mbele ya Allah, Hadhrat Abu Bakr Siddik r.a. aliposema kwa Mtume saw ya kuwa wakati ambapo ahadi ya kupata ushindi ipo tena kuna sababu gani ya kufanya maombi mengi hapo Mtume saw akamjibu ya kwamba Yeye ni Mkwasi yaani yawezekana kuwa katika ahadi ya Mwenyezi Mungu yawe masharti yasiyojulikana.

Baraka za Taqwa yaani uchaMungu

Basi kwa siku zote tuwe tukiangalia yakuwa tumepata maendeleo kiasi gani katika mambo ya uchaMungu na utakaso na kiwango chake cha kupima ni Kurani Tukufu. Alama moja ya wachaMungu ielezwayo na Mwenyezi Mungu ni hii yakuwa Yeye Anamtosha katika mambo yote ya dunia kama Alivyosema katika sura At-Talaaq aya 3, 4 na anayemwogopoa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu Humtengenezea njia ya kuokoka, na Humpa riziki kwa mahali asipopatazamia; yaani hii pia ni alama moja ya mchaMungu ya kuwa Mungu Anamtosha kutokana na mahitaji yake, kwa mfano mfanyabiashara mmoja anafikiri yakuwa kazi yake haiwezi kusonga mbele bila kusema uongo naye anatoa udhuru katika hilo lakini jambo hili si kweli kamwe. Mwenyezi Mungu Anamtosha mchaMungu kuwa mlinzi wake na kumwepusha kutoka mambo ambayo yawe yanamlazimisha kutenda kinyume cha haki.
Kumbukeni ya kuwa mtu akimwacha Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu pia Atamwacha na Akimwacha Yeye basi lazima shetani atajiunga naye.
Msifahamu ya kuwa Mwenyezi Mungu ni dhaifu, Yeye Ana nguvu kweli kweli. Mtakapomtegemea Yeye katika jambo fulani, lazima Yeye Atawasaidieni na anayemtegemea Mwenyezi Mungu, basi Yeye Humtoshea; pia ikumbukwe ya kuwa watu ambao walilengwa awali katika aya hizi walikuwa watu wa dini, fikra zao zote zilikuwa kwa ajili ya dini na mambo ya dunia walimwachia Mwenyezi Mungu tu, hivyo basi Mwenyezi Mungu Aliwafariji kwa kusema ya kuwa Mimi nipo pamoja nanyi. Ilmuradi Baraka moja ya Taqwa ni hii ya kuwa Mwenyezi Mungu Anamwokoa mchaMungu kutoka mabalaa yale ambayo yanaweza kuingilia kati ya mambo ya dini.
Mwenyezi Mungu Atusaidie kuzingatia na kutekeleza hayo yote. Amin.

MALFOOZAT JALADA LA KWANZA UKURASA NAMBA 7- 8.
MFASIRI SHEIKH WASEEM AHMAD KHAN , TABORA

(Malfoodhaat ni mazungumzo ambayo Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliyafanya katika maeneo na nyakati mbalimbali na yakahifadhiwa kwa maandishi na Masahaba zake r.a. - Mhariri).

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo
Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Mtaheshimika kwa matendo sio maneno

Kutoka uk. 1

wa kuwategemea wengine. Na kwa ajili ya urekebishaji wa matendo, mwegemeo huu ni wa aina mbili au kuna haja ya kuwa na miegemeo ya aina mbili. Mmoja ni wa usimamizi, na wa pili ni wa shinikizo. Wa usimamizi ni huu kwamba daima awe chini ya uangalizi ili isije popote akafanya kitendo kibaya.

Usimamizi wa aina hii upo hata katika masuala ya kidunia. Wazazi huwasimamia watoto majumbani. Mashuleni, walimu, mbali na kufundisha, hufanya pia kazi ya usimamizi. Wakati mwingine wafanyakazi wa serikali nao hufanya usimamizi na husema kuwa sisi tutasimamia. Barabarani zimewekwa kamera za kudumu kwa ajili ya usalama barabarani pamwe na mabango ya aina mbali mbali, hii pia ni aina fulani ya usimamizi.

Wale watoto wanaoteswa na wazazi wao, wazazi hao pia huonywa wakiambiwa kuwa sisi tutafanya usimamizi kama mtaendelea kuwasumbua watoto. Hapo ile idara ya kuwalea watoto hutahadharisha kuwa sisi tutawachukua watoto hao. Hili ni jambo la kawaida sana katika nchi hizi zilizoendelea. Bali kwa rai yangu haijuzu kwa kiwango fulani katika masuala haya ya watoto, ambapo wazazi kwa kuiogopa idara hii, huogopa hata kuwarudi ipasavyo watoto wao na matokeo yake, wakati mwingine, baadhi ya watoto huharibika.

Hivyo katika masuala ya kidunia, wakati mwingine usimamizi huu huwa chanzo cha hasara. Kisha katika mahusiano ya mume na mke, kutokana na migongano fulani huwa kunakuwepo na usimamizi. Pia kuna usimamizi wa wahalifu.

Kwa vyovyote vile, makusudio yote ya simamizi hizo, ni kuyazuia mambo yale yanayoleta uharibifu, au makusudio yake ni kurekebisha. Hivyo, kwa vyovyote vile, usimamizi ni njia moja wapo ya urekebishaji katika sheria ya kila jamii. Na dini pia, inatuelekeza kwenye usimamizi wa aina hii, kwa ajili ya urekebishaji wa vitendo, na mwanadamu huyaepuka mambo mengi ya makosa, pale jamii inapomsimamia, wazazi nao husimamia ndani ya wigo wao.

Hii ni kazi ya wabashiri kusimamia katika maeneo yao na ni muhimu kwa uongozi mzima wa Jumuiya kusimamia katika maeneo yao. Na wakati kukiwepo pia na fundisho hili la Islam, kwamba kila msimamizi ataulizwa kuhusiana na usimamizi wake, basi sio tu hurekebika yule anayesimamiwa, bali hata wale wanaosimamia watarekebika. Hivyo kwa hali yoyote ile, usimamizi ni njia yenye athari kwa ajili ya kila marekebisho ya matendo.

Jambo la pili lililo la muhimu kwa ajili ya marekebisho ni shinikizo. Hapa laweza kuingia katika moyo wa mtu wazo hili kwamba upande mmoja tunasema kuwa hakuna kulazimishana katika masuala ya dini, upande wa pili tiba ya urekebishaji wa matendo inayoshauriwa ni ya ulazimishaji. Hivyo iwe wazi kwamba ulazimishaji huu sio wa kulazimisha kuiacha au kuikubali dini. Kila mtu anao uhuru wa kuichagua dini yoyote aitakayo na wa kuiacha dini yoyote aitakayo. Islam yaitoa hiari hii kwa uwazi kabisa.

Hapa ulazimishaji ni huu kwamba baada ya kujielekeza kwenye upande wa dini kisha kutoshikamana na maagizo yake au kuyavunja. Upande mmoja kujisema kuwa wewe ni sehemu ya nidhamu ya Jumuiya na kisha kuzivunja kanuni za nidhamu, kama jambo hili linatendeka.....

Basi nguvu itatumika, na hapa hii ndiyo maana ya "Jabar" (kutumia nguvu). Kama unataka kuishi huku ukiwa sehemu ya nidhamu, basi ni lazima pia ufuate mafundisho, la sivyo unaweza kupewa adhabu, kutozwa faini au kuwekewa baadhi ya vikwazo. Na shabaha hasa ya kuchukua hatua hizi zote ni kufanya marekebisho, ili udhaifu wa nguvu ya kimatendo uweze kuondolewa.

Katika Jumuiyya pia, nidhamu ya Jumuiyya inapotoa adhabu yoyote, kwa hakika huwa inalenga tu kufanya marekebisho, wala haitaki kumfedhehesha au kumtaabisha yeyote. "Jabar" hii inapatikana hata katika kanuni za serikali, ambapo watu huwa wanaadhibiwa, wanafungwa jela, wanatozwa faini na wakati mwngine hata upigwa. Na lengo huwa ni hili tu kwamba amani istawi katika jamii na wanaotaka kuwadhuru wengine wasipate kufanikiwa katika mipango yao. Bali baadhi ya wakati, mtu anapewa adhabu kwa sababu ya kujiumiza mwenyewe, lakini katika kutoa adhabu hii, zinatumika njia mbali mbali za kufanya marekebisho. Kama kuna yeyote anayenyongwa, basi " Jabar " hii hufanyika kwa sababu muuaji alimwua mtu. Na kama wauaji wangepewa uhuru, amani ya jamii ingevunjiliwa mbali na kuzaa wauaji wengine wengi. Kwa hiyo, kutokana na adhabu ya kifo ya mauaji, watu wenye jadhba na walio na mwelekeo wa kuua hujirekebisha au kujiepusha na kitendo hiki.

Kwa vyovyote vile, " jabar" (kutumia nguvu), ni njia mojawapo ya urekebishaji inayotumika pia duniani. Adhabu zinazotolewa na serikali duniani, hazihusikani na imani, lakini mtu anayefuata dini anapofanyiwa jabar, na sawa na nidhamu, anapopewa adhabu ya aina yoyote au kutozwa faini au kuwekewa vikwazo fulani; kama vile Jumuiya kukataa kupokea mchango wa mtu huyo, bila shaka anazuiwa kwa nguvu, lakini pamoja na hayo aelekezwe kwenye matendo mema, naye akiyatekeleza kwa nia ya kuepuka adhabu au hasira ya Khalifa au ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, basi taratibu imani huanza kuzalika moyoni mwake na kuongezeka.

Na watu wa aina hii, hugeuka kuwa watu wanaoachana na ubaya na kuanza kutenda mema kwa furaha.

Hivyo basi, Daima ikumbukwe ya kwamba, kwa kuzoea kutenda matendo mema, huwa zinatumika njia mbali mbali, ambapo bila ya kuzifuata njia hizo, mafanikio katika kuyarekebisha matendo hayawezi kupatikana. Basi kuzifuata njia hizo ni muhimu sana, yaani kuimarisha imani na kutafuta elimu sahihi, na mambo haya mawili yalisha elezwa katika hotuba iliyopita.

Na kusimamia na kutumia nguvu ni mambo ambayo nimeyataja sasa hivi kwa ajili ya kupata nguvu ya kutenda matendo mema. Ni vigumu kujirekebisha bila kuzifuata njia hizo nne.

Tuchunguzapo kwa undani, tunabaini ya kwamba duniani kuna kundi moja la watu wasio na nguvu ya kiimani mioyoni mwao, yaani hawana kile kiwango kilicho muhimu kwa ajili ya mtu kujirekebisha kimatendo. Watu wa namna hii wakijaziwa nguvu ya kiimani mioyoni, matendo yao hurekebika. Na kuna kundi la watu wanaozama katika maasi kutokana na kukosa kuelewa, nao wanapaswa kutafuta elimu sahihi. Kundi jingine ni la watu wanaowahitaji wengine kwa ajili ya kutenda matendo. Hao ni watu wa aina tatu ambao wanaweza kusaidiwa kwa namna mbili. Kwanza kwa kusimamiwa, ambako maelezo yake nimeyaeleza hivi sasa kuwa mtu akisimamiwa huachana na maovu na kuelekea kwenye kutenda mema. Lakini kundi lile lililo baya sana wala halidhibitiwi hata na usimamizi, haliwezi kujirekebisha mpaka liadhibiwe. Hivyo basi, ni muhimu kuzitumia njia hizo zote nne kwa ajili ya marekebisho ya Jumuiyya. Na ni lazima kila mmoja atibiwe kulingana na ugonjwa wake.

Ni muhimu kulikumbuka jambo hili kwamba, katika zama ambapo dini inakuwa haina serikali au nguvu, tiba hizi nne huwa ni za lazima. Basi kama ilivyoelezwa katika hotuba iliyopita kwamba sawa na tiba ya kwanza, ni muhimu kuiimarisha imani kwa malezi mazuri. Na kwa kufikia hilo, zibainishwe ishara za Sayyidna Ahmad as, wahyi aliofunuliwa, uhusiano wake wa karibu na Allah na mapinduzi ya kiroho aliyoyaleta katika wafuasi wake. Watu wafahamishwe faida za kujenga ukaribu na Allah.

Kama nilivyosema katika hotuba iliyopita ya kwamba, katika zama hizi ambapo shetani anafanya mashambulizi kwa nguvu, kuna haja kubwa sana ya kuyaeleza mambo haya na yatajwe mfululizo na mara kwa mara. Kuna haja ya kubainisha namna ya kupata mapenzi ya Mwenyezi Mungu na yule anayejaliwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu anatendewa namna gani na Mwenyezi Mungu. Hadhrat Masihe Mauud as ametueleza vipi kuhusiana na hayo. Wanajumuiyya wapya wa mataifa mbali mbali, kama vile waafrika na waarabu, wananiandikia matukio yao ya mabadiliko yanayotokea nafsini mwao na kuongezeka imani baada ya kusoma vitabu vya Sayyidna Ahmad as. Bila shaka, baada ya kuvisoma vitabu, waliyarekebisha makosa yao ya kiitikadi na kuongezeka elimu na wakaziona njia mpya za imani, lakini uimara wa imani ulizalika ndani mwao baada ya kuziona ishara za Hadhrat Masihi aliyeahidiwa as na kufahamu uhakika wa wahyi wake na uhusiano wake na Allah. Kisha Allah naye akawathibitishia ukaribu Wake kwa kuwaonyesha baadhi ya ishara.

Hadhrat Muslih Mauud (mwana aliyeahidiwa ra) akieleza umuhimu wa ishara za Sayyidna Ahmad as, funuo zake na uhusiano wake na Allah, pia kwa kuelezea umuhimu wa jambo ambalo, liwe lenye kungarisha zaidi miyale ya imani kwenye mioyo yetu, alisema kwa mtindo wake kama ifuatavyo; "Hata kama Hadhrat Issa as awe amekaa mbinguni akiwa hai, maana kukaa kwake hai mbinguni hakuleti madhara sana jinsi kuletavyo madhara kwa kufa kwa Mwenyezi Mungu mioyoni mwetu. Basi kuna faida gani ya kuendelea kulisisitiza jambo hili la kifo cha Nabi Issa as, ilhali upande wa pili mnamwacha Mwenyezi Mungu Afe ndani ya mioyo ya watu na wala hamjitahidi kumhuisha. Mwenyezi Mungu ndiye Mzima na Mhifadhi wa milele, Naye Hafi asilan, lakini anakufa pia, kutokana na tabia za baadhi ya watu.

Hadhrat Muslih Mauud ra anaeleza kisa kimoja kihusikanacho na Hadhrat Khalifa tul Masih wa kwanza r.a. ya kwamba, mwalimu wake mmoja aliyekuwa mkazi wa Bhopal, anasema kwamba, safari moja aliona katika njozi ya kwamba kuna daraja moja lililopo nje kidogo ya mji wa Bhopal, Bhopal ni mji unaopatikana nchini India, ambapo kuna mtu mwenye ukoma, pamoja na ugonjwa huu wa ukoma, alikuwa pia ni kipofu, pua yake imekatika, vidole vyake vimekwishaharibika na mwili wake wote umejawa na usaha, nzi wamemzunguka pande zote. Yeye anasema ya kuwa mandhari hii ilinikera sana, nami nikamwuliza; mzee wewe ni nani? Yeye alisema mimi ni mungu.

Nilipolisikia jibu hilo mimi nikashikwa na bumbuazi nami nikasema wewe ni mungu!

Mitume wote waliokuja duniani wameendelea kusema mpaka leo kwamba Mwenyezi Mungu ni Mzuri kuliko wote na hakuna kitu kilicho kizuri zaidi kushinda Yeye. Sisi ambao tunampenda Mwenyezi Mungu, basi je hii ndiyo sura yake? Yeye akajibu ya kuwa yale yote yasemwayo na mitume ni sahihi kabisa. Mimi si Mungu wa kweli, bali mimi ni mungu wa wakazi wa Bhopal. yaani katika mitazamo ya wakazi wa Bhopal, mimi nafahamika jinsi nilivyo sasa, yaani watu hao hawamthamini Mwenyezi Mungu hata kidogo.

Basi Mwenyezi Mungu Hafi kamwe, lakini wakati ambapo binadamu huwa anamsahau, basi kwa ajili yake, Yeye (Mungu) anakuwa amekufa. Hapa ningependa pia kuwafahamisha vijana kwamba wao wasielewe kutokana na hayo ya kuwa Mungu Ameshika Anashika sura hiyo mpya kwa kuona tabia za watu na kazi imeisha hapa, kwa hakika sura hii ni ya wale waliomwacha Mwenyezi Mungu, kama vile mtu aonavyo picha yake kwenye kioo, na huu ndio uhakika ya kwamba, picha yake ndiyo inayoonekana. Sura hii aliyoiona katika ndoto yake ilikuwa ni kioo chao, nao kiroho wakawa wenye ukoma na watu kama hao mwishowe huuona mwisho wao. Mungu Apishe

Endelea uk. 4

Mtaheshimika kwa matendo sio maneno

Kutoka uk. 3

mbali, Mwenyezi Mungu Hakujitenga nao kwa kufa, bali wale ambao wanamchukulia Mwenyezi Mungu kama mfu, wakati mwingine Mwenyezi Mungu Huwaadhibu watu hao humu duniani. Mwenyezi Mungu Hakai tu pembeni, bali katika dunia hii hii huwaadhibu watu kama hao, na katika sehemu mbali mbali, Mwenyezi Mungu Ameeleza mwisho wa watu hao waliomsahau Mungu ya kuwa wataingia katika jahanamu. Basi kutokana na mfano huo, isieleweke ya kwamba kumwacha Mungu au kumfahamu kuwa na udhaifu hakutaleta shida yoyote na jambo kuishia hapo, hapana, Mwenyezi Mungu ni Mwenye kulipiza kisasi na Mwenye kuadhibu na ghadhabu yake inaposhuka hakuna yeyote anayeweza kusimama mbele yake, basi kwa msingi huo, jambo hili si la kawaida ya kwamba tukimsahau Mwenyezi Mungu basi biashara imeisha.

Hadhrat Muslih Mauud ra anasema ya kwamba ni jambo la ajabu kwamba masheikh wetu wanajaribu kumfisha Hadhrat Issa as, lakini pamoja na hayo hawajaribu kumhuisha Allah Taala, hawaleti hamasa ambayo iwe sababu ya kumwelewa na kumtambua Allah Taala. Juhudi yetu haswa iwe ya kumhuisha Allah Taala na kuwa na mahusiano madhubuti pamoja naye. Kama mahusiano yetu na Allah Taala yako hai, basi wale wanaomfahamu Isa kuwa hai, na waendelee tu kupiga makelele watakavyo, imani yetu haitaharibika kamwe, kwani Mwenyezi Mungu Yu pamoja nasi kila wakati na Atatusaidia.

Basi hakuna shaka ya kuwa, elimu ihusuyo kifo cha Nabi Issa, Utume kuendelea na mambo mengine yanayohusikana na itikadi lazima yapatikane na pia ni muhimu kusimama imara juu yake kwa dalili, na sio bila dalili. Lakini kwa ajili ya urekebishaji wa matendo, tutalazimika kujenga mahusiano na Allah Taala na katika kulifanikisha hilo, tutapaswa kutumia njia ambazo Sayyidna Ahmad as ametuonesha katika zama hizi, tutalazimika kufuta tofauti baina ya kauli na matendo yetu. Pia tujichunguze nafsi zetu kuhusiana na kile tunachowaambia wengine, kwamba ni kwa kiasi gani tunakitekeleza hicho.

Leo, kwa fadhila za Mwenyezi Mungu, Jumuiya inavyo vyuo vya Jamia Ahmadiyya katika nchi mbali mbali duniani ambamo masheikh na wabashiri wa Jumuiyya wanaandaliwa na vijana wengi wanaendelea kujiunga na vyuo hivyo , hususan huko Pakistani vijana ambao wengi wao huwa ni waqfe Nau , wanakuja kwa wingi ili kujiunga na Chuo cha Jamia Ahmadiyya, wakati mwingine hutokea hivi kwamba, idadi kubwa husababisha kiwango kishuke chini, na wakati mwingine mifano hii hujitokeza kutokana na kutokujitahidi katika kujipatia kiwango cha kiroho.

Bali wengine, kutokana na baadhi ya tabia mbaya, na kutokuwa na elimu sahihi ya kwamba mbashiri na mwalimu wanapaswa kuwa na utukufu wa aina gani, wanapokosea kwa namna fulani, basi huwa wanafukuzwa Jumuiya. Basi zama zijazo ni zama za maendeleo ya Jumuiyya ya waislamu waahmadiyya inshallah, kwa ajili ya kuzifanyia zama hizi maandalizi, wale wanaotarajia kuwa wabashiri na waalimu, wanapaswa kujiandaa kwa nguvu zote, kwani kazi watakayokabidhiwa sio ndogo. Kuanzia sasa wajitahidi kujenga uhusiano maalumu na Mwenyezi Mungu na kujitahidi zaidi kuliko awali. Wayazingatie mafundisho ya kweli ya kiislamu aliyoyabainisha Sayyidna Ahmad as waziwazi kwa mara nyingine tena na ishara zake alizotuonesha. Msiwe tu mkijikita katika kukumbuka tu hoja na dalili.

Kuna mwanazuoni mmoja aliyeniandikia kutoka Qadiyan kuhusiana na mikutano ya hadhara iliyokuwa ikifanyika kwa lengo la kuwajibu wapinzani nchini India, ambayo kwa sasa haifanyiki, kwamba; Sisi katika mikutano hiyo tulikuwa tukiwashambulia wapinzani kwa mashambulio makali yaliyokuwa yakiwanyamazisha kabisa wapinzani, ambayo moja baada ya jingine lilikuwa likiwamaliza. Sawa, hili ni jambo zuri kwamba walikuwa wakifanya hivyo, yatupasa kuwajibu wapinzani, bali upingaji wake urudishwe kwao kwa dalili. Lakini jambo hili ni lazima, na muhimu zaidi kuliko hili ni kwamba waalimu, wahubiri na wabashiri wetu wakielewa shabaha hasa ya ujio wa Hadhrat Ahmad as, wanatakiwa kupata maendeleo ya kiroho kiasi hiki kwamba kila mmoja wao awe ishara. Na kwa kufikia lengo hilo , inapaswa kufanya jitihada. Na kwa kuona mfano huu , watu wajiunge na Jumuiyya ya waislamu waahmadiyya kwani wakati mwingine watu wanajiunga na Jumuiyya kwa kuona mifano mizuri. Lakini hapa nasikitika kusema kwamba, kiwango hiki hakijazalika, ndiyo maana waalimu wengi walisimamishwa kazi huko nchini India na ilionekana kuwa baadhi yao walitawaliwa na mapenzi ya kidunia.

Hivyo basi, huyu aliyeandika barua hii, na kila mmoja wetu ajichunguze kuwa ana majukumu gani? waalimu na wabashiri walitazame jambo hili kwamba wao wamejitahidi kwa kiasi gani ili kuzalisha imani mioyoni. Hatupaswi kutosheka na kuishia kwenye kuziathiri nyoyo za watu kwa hoja na dalili, au kwa kuwafunga vinywa masheikh wasiokuwa waahmadiyya, bali kwa ishara hai na miujiza ya Mwenyezi Mungu tuliyo nayo , tuioneshe dunia uwepo wa Mwenyezi Mungu. Tuishinde mioyo ya watu kwa ushuhuda wa kimatendo wa Mwenyezi Mungu ulio pamoja na Hadhrat Ahmad as.

Hadhrat Musleh Mauud ra alipiga mfano mmoja kwamba baada ya jua kuchomoza, kama yeyote akimwuliza mtu kwamba unayo dalili gani kuwa jua limechomoza, hapo mwingine akianza kutoa dalili zake kuwa jua linachomoza saa fulani, na sayansi inasema jambo fulani na kadha wa kadha. Hazrat Musleh Mauud anasema kuwa huyo anayetoa dalili anakuwa pia ni jahili kwa kuanza kutoa dalili, badala yake mtu huyo alitakiwa auinue uso wa huyo mwulizaji, kwa kumshika kidevuni, ili aweze kuliona jua, maana jibu la swali lake la kijinga ni uwepo wa jua lenyewe.

Basi, siku hizi Mwenyezi Mungu pia Amejidhihirisha kwetu na Amejionesha waziwazi mbele ya dunia kwa sifa Zake zote na kujidhihirisha kwa uzuri Wake wote kupitia Sayyidna Ahmad as. Basi badala ya kujifanya mjinga anayetoa dalili za uwepo wa jua, uthibitishe ukweli huu kwa ishara mpya zinazodhihiri kwa kupitia Sayyidna Ahmad as na ushuhuda wa kimatendo wa Mwenyezi Mungu ulio pamoja nasi kila saa.

Lakini jambo la msingi ni hili tu kwamba mzifanye hali zenu ziendane na ridhaa ya Mwenyezi Mungu na kuimarisha nguvu ya kimatendo ya Jumuiyya kwa kuyaweka mambo haya mbele ya watoto, wazee na wanawake wa Jumuiyya mara kwa mara. Waambieni kwamba jalali ya Mwenyezi Mungu imedhihiri vipi kwa kumpitia Sayyidna Ahmad as, na waelekezeni kwenye njia za kupata ukaribu na Allah na wafahamisheni kuwa wanawezaje kupata mapenzi ya Allah. Kisha mtaona kwamba wale vijana walioielekea dunia, watakuwa wenye kuinama mbele ya Mwenyezi Mungu. Hapo hakutakuwa na wabashiri au wanazuoni wachache wanaowashinda kwa kishindo masheikh wapinzani, bali mifano hii mizuri watakayoionesha watoto, wazee na wanawake itakuwa yenye kuivutia dunia.

Hivyo awali ya yote kuna haja kubwa sana ya kuyarekebisha matendo yetu. Baada ya kujiunga na Sayyidna Ahmad as, kitu kinachohitajika zaidi kuliko vyote ni utii mkamilifu kwa Ukhalifa. Na hicho ndicho kitu kitakachokuwa sababu ya kuiimarisha Jumuiya na kuleta maendeleo ya kiroho. Jumuiya inapaswa kufahamu utambuzi, elimu sahihi na maarifa ya Ukhalifa kwa namna hii kwamba wanajumuiyya wote wawe wenye kulitii kila agizo la Khalifa bila kuwa na wasiwasi wowote moyoni, na wasishikwe na wahaka kwa kusikia jambo lolote. Kuwaelimisha wanajumuiyya kuhusu uelewa na maarifa ya kweli ya Ukhalifa ni jukumu muhimu sana kati ya majukumu ya wabashiri, na viongozi wengine pia wanapaswa kujielekeza kwenye jambo hili.

Wakati mwingine mifano ya namna hii inajitokeza inaposemwa kwamba Khalifa alitenda jambo fulani lisilo sahihi, au alifanya uamuzi usio sahihi, au wakati mwingine hukumu za ofisi ya Qadhi pia zinapingwa, au kwa nini mtu fulani alipewa kazi fulani, bali badala yake mtu fulani alitakiwa apewe kazi hiyo, au Khalifa anawajua sana watu fulani na fulani na wengine amewafumbia macho juu ya kuwa na taarifa zao.

Wanaoongea mambo kama haya huwa ni wachache sana lakini huharibu mazingira. Kama wabashiri na wenye vyeo wa kila ngazi, jinsi nilivyotangulia kusema kwamba viongozi wote wa Jumuiyya na wa matandhim, wakilielewe vizuri jukumu lao hili, basi wasiwasi unaozalika katika baadhi ya mioyo, hautazalika asilani. Ni wajibu wa wabashiri kuwafahamisha wanajumuiyya kwamba baraka zote zimo katika nidhamu. Mwenyezi Mungu Anapotaka kuwalaani watu fulani, Anaondoa nidhamu kati yao.

Hivyo, kila mmoja atakapokuwa ameyafahamu mambo yote haya, basi wale wanaoteleza wataepuka kuteleza. Watu wanaojidhani kuwa ni wenye akili sana hupatikana siku zote, hata kama ni wachache na huongea mambo kwa kukaa hapa na pale kuwa Khalifa sio Mungu na anaweza kufanya kosa pia kama afanyavyo kosa mtu wa kawaida. Ni sahihi kabisa lakini Hadhrat Muslihe Mauud ra alitoa jibu zuri la jambo hili na ikiwa Ukhalifa ni wa kweli yaani kama tunaamini kuwa Ukhalifa ni neema iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu, basi jibu hili la Hadhrat Muslihe Mauud ra ni la wakati wote na zama zote.

Hadhrat Muslih Mauud ra alisema “Mwenyezi Mungu Anasema kuwa tunayasimamisha duniani mambo wanayoyaamuru makhalifa naye Anasema; “walayumakkinanna lahum diina humulladhirtadhaa lahum” yaani dini ile na kanuni zile ambazo makhalifa wanataka kuzisimamisha duniani, Sisi Tunasema kwa kula kiapo cha dhati yetu kwamba, bila shaka Tutazisimamisha duniani”. Hivyo basi, kila mwanajumuiyya awe anayafahamu vizuri mambo hayo na hii ni kazi ya wabashiri na wenye elimu, kwamba wayapenyeze mambo haya katika moyo wa kila mwanajumuiyya.

Basi zingatieni sana jukumu hili na kufanya kila jitihada ya kuwadhihirishia watu neema na baraka za Sayyidna Ahmad as na kutaja mara kwa mara ishara hai za Mwenyezi Mungu. Wajulisheni watu namna ya kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu na wafahamisheni watu kuwa kumtii Khalifa katika kila hali na kuifuata nidhamu kuna umuhimu wake mkubwa, ambao kila mmoja awe anauelewa vizuri. Hivyo hayo yatakapotendeka basi wasiwasi wa moyoni pia utaondolewa. Na kwa njia hiyo wale ambao wataondoa wasiwasi wao au watakaoondolewa wasiwasi wao, na idadi yao itaongezeka kwa kiasi hiki, kwamba kila fitina itajifia yenyewe. Mabadiliko mazuri ya matendo ya kila namna yataonekana ndani ya Jamaati na hii ndio shabaha hasa ya kuja kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Ikumbukwe kuwa, tunapaswa kuyajua masuala ya kifo cha Nabi Issa na ya khatme nubuwwat (kuendelea kwa utume) na haya yanahitajika kwa ajili ya kujibu maswali ya wapinzani lakini, juhudi kubwa inahitajika kwa ajili ya kuendeleza vitendo na maarifa juu ya dhati ya Mwenyezi Mungu katika Jumuiyya. Basi tunalazimika kufanya juhudi kubwa zaidi kwa ajili ya jihadi ya ndani kuliko zile ambazo zinahitajika kwa ajili ya jihadi ya nje .

Mabadiliko yetu ya matendo na utakaso wetu wa roho yataleta maendeleo makubwa kuliko mahubiri, inshaallah Taalah. Usemi huu wa Hadhrat Musleh Maud r.a. una thamani

Endelea uk. 8

Wasifu wa Marehemu Mzee Mubarak Athumani

Na Mwandishi wetu

Marehemu mzee Mubarak Athuman alizaliwa mwaka 1930 takribani miaka 83 iliyopita Mkoani Mbeya Wilaya ya Kyela.

Hakupata bahati ya kulelewa na baba yake mzazi kwani baba yake alifariki yeye akiwa bado ananyonya, hivyo kwa kiasi kikubwa malezi yake alipatiwa na mama pamoja na wajomba zake ambao walikuwa wanaishi Wilaya ya Songea kijiji cha Liongo Peramiho Mkoani Ruvuma.

Mzee Mubarak hakuwahi kusoma shule lakini alikuwa na kipawa cha ajabu sana, kwa kufundishwa tu na wenzake ambao walibahatika kwenda shulekatikamichezoyaoaliweza kujua kusoma na kuandika jambo lililowastajabisha watu, na wengine walifikiri kuwa aliwahi kusoma shule.

Alipofikia umri angalau wa kuanza kujitegemea alienda Mkoani Morogoro wilaya ya Kilosa, ambako kwa kiasi kikubwa maisha yake yalikuwa chini ya mtu baki, na huko ndiko alikojifunza fani yake ya udereva ambaye aliweza kudumu naye mpaka umauti wake.

Mzee Mubaraka alipenda sana kutusimulia watoto wake visa vya aina mbalimbali enzi wa ujana wake, alitusimulia ya kwamba akiwa na fani yake hiyo ya udereva pia aliweza kufanya kazi mbalimbali tofauti na fani yake hiyo, alishawahi kufanya kazi kwa muhindi ambaye yeye na familia yake walimpenda sana mzee Mubarak.

Alitusimulia ya kwamba siku moja alitumwa sokoni na huyo bosi wake muhindi kununua nyama, alipofika sokoni akakutana na jamaa anatafuta dereva wa basi lake la abiria hivyo wakakubaliana kwamba yeye mzee Mubarak awe dereva wake sasa kikwazo ile kazi aliyokuwa nayo afanyeje ili aweze kuachana nayo na ukizingatia alikuwa anapendwa sana na bosi wake, akafikiri! akaamua kwamba nimetumwa nyama sasa nitawanunulia utumbo.

Kweli alipofika na utumbo wakamuuliza kwa ukali mbona umeleta utumbo wakati tulikutuma stake? Akawajibu kwani utumbo si nyama kwanza na kazi yenyewe basi! Akaacha pale pale na kuondoka zake kuelekea kwa Yule jamaa wa basi na kuanza kazi.

Pia mzee Mubarak katika maisha ya ujana wake kabla ya ndoa zake alishawahi kufungwa gerezani kwa kosa la kutolipa kodi ya kichwa. Alitusimulia ya kwamba; Akiwa gerezani walikuwa wafungwa wote wanakawaida ya kupelekwa msituni kwa ajili ya kukata na kubeba magogo ya kuni, wakiwa huko msituni huwa wanapangwa wawili wawili mmoja anakata na mwingine anabeba kupeleka katika gari, wanafanya zamu akichoka wa kukata aliyekuwa anabeba yeye sasa anakata, na mwenzake anabeba. Sasa siku hiyo yeye akawa wa kwanza kubeba kupeleka

katika gari, anasimulia ya kwamba siku hiyo likampata wazo la kutoroka, huku akijiuliza napata tabu kwa kosa gani kubwa nililofanya kutokulipa kodi tu nipate shurba zote hizi! Ingawaje walikuwa kwenye msitu mnene na hakujua huo ni msitu gani na wala hakufahamu umbali wa walikotoka mpaka msituni hapo, lakini akakata shauri leo lazima nitoroke. Basi! Akabeba mara ya kwanza kupeleka katika gari, mara ya pili akapeleka akiweka katika gari na yeye mwenyewe kuanza kukimbia kuelekea asikokujua, anasimulia ya kwamba alikimbia kwa kasi katika hali ya kuinama ili asionekane huku akipishana na wanyama kwa hofu kwa muda mrefu na aliendelea kukimbia mpaka jua linazama bado yeye yupo ndani ya msitu ule ulio na wanyama wakali. Jua lilipozama na kuanza kuingia kiza, akaona bora achimbe shimo akajifukia mwili mzima na kubakiza kichwa tu ili kujilinda dhidi ya wanyama wakali, alilala katika hali hiyo kwa usalama mpaka asubuhi na kuendelea na safari yake huku akiwa na njaa kali sana na kiu cha maji. Alisafiri siku hiyo mpaka usiku hatimaye akafika katika mji, pale akaelekea moja kwa moja mpaka kwa mjomba wake ambaye waliachana siku nyingi akamkuta, wakasalimiana kisha akaanza kumweleza mkasa mzima uliomkuta, baada ya hapo mjomba wake akaagiza iandaliwe chai cha ajabu baada ya kuja ile chai akawa anainywa peke yake hata bila ya kumkaribisha mgeni wake huyo, kitu kilichomshangaza sana mzee Mubarak hatima yake ikabidi aage na kuondoka zake huku akiwa na njaa yake.

Njiani akakutana na mtoto anakula hindi mzee Mubarak akamuomba Yule mtoto lile hindi, Yule mtoto akakataa kumpa kwakuwa mzee Mubarak alikuwa na njaa kali sana uzalendo ukamshinda hivyo ikabidi amnyang'anye Yule mtoto lile hindi na kukimbia huku akimwacha Yule mtoto analia.

NDOA YAKE

Sawa na maelezo yake mwenyewe marehemu inaonesha kuwa ndoa yake ya kwanza alifunga mwaka 1950 ambayo haikudumu kwa muda mrefu.

Baada ya kuvunjika ndoa hiyo alijaaliwa kufunga ndoa nyingine na Bi. Madawa Hamisi mwaka 1960 na mwaka 1970



Mzee Mubarak Athumani enzi za wa ujana wake

alifunga ndoa nyingine na Bi. Zuhura Suleiman.

Bi Madawa Hamisi amejaaliwa kuzaa naye watoto nane kati ya hao watatu ndio wapo hai

Bi. Zuhura Suleiman amejaaliwa kuzaa naye watoto kumi na nne kati ya hao tisa ndio wapo hai,

Sawa na maelezo yake marehemu katika maisha yake ya awali alikua mlevi wakupindukia kiasi hiki kwamba alikuwa hawezi kupitisha siku bila ya kuywa angalau chupa nne za bia na kushushia packet moja la sigara.maisha yake kabla ya jamaati yamejaa visa vyenye ukorofi kwa sababu alikuwa si muongeaji sana, wakina mama wanatusimulia kwamba alikuwa hasa hasa akionesha vitendo tu vya kuchukua hatua mkononi ndio maana katika ujana wake baadhi ya watu walimuita mzee makofi.

MAISHA YAKE BAADA YA KUJIUNGA NA JUMUIYYA YA WAISLAMU WAAHMAMADIYYA

Marehemu mzee Mubarak Athuman alijaaliwa kujiunga na Jumuiyya ya Waislam Waahmadiya mnamo mwaka 1977, kwa kuhubiriwa kwa jitihada kubwa na dada yake aitwaye Fatma bint Athuman ambaye sasa naye ni marehemu.kutokana na sifa ya bibi huyo ya uchamungu ambapo waahmadiyya wengi hasa wa songea mjini wanajua sifa na jazba ya mapenzi yake ya jamaati huyu bibi kiasi kwamba jazba hii ilmpelekea kuwaelezea watoto wake umuhimu wa mpango wa waqfu nao na akasema, natamani kama wajukuu wangu wote wangeliingia kwenye mpango huu na kusababisha mjukuu wake mmoja awe katika waqfu na alikuwa akija nae yeye mwenyewe msikitini ,dada yake huyo alifariki bila ya kuugua. Siku hiyo aliyofariki walikuwa wametoka shamba yeye, mke wa mwanaye na mjukuu wake, baada ya kuandaa chakula na kula hatimae wote walikubaliana kurudia kupika tena chakula kingine baada ya kile cha kwanza kutoshiba hivyo marehemu aliwaambia kipindi mnaandaa ngoja mimi nikasali kabisa kwani muda wasala ulikuwa umefika, akiwa chumbani kwake akijisalia sala ya Insha chumbani kwake katika hali sajda ndipo alifariki dunia (Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea) chakula kilipokuwa tayari na kuona muda mrefu unapita ndipo mjukuu wake mmoja alipoamua kumfuata alipofika akagundua kuwa bibi yake hayupo tena duaniani. Kifo ambacho nakumbuka marehemu mzee alipokuwa anatoa mchozi alisema nalia hasa hali aliyokufa nayo dada akiwa anasali akasema hii ndio hali bora ya kifo ukiwa unamkumbuka mola wako.

Hivyo kulingana na sifa za bibi huyo aliweza kufanikisha kumshawishi mzee mubaraka kujaza bayati mwaka huo 1977 sawa na taarifa iliyopatikana kutokana na tabia hiyo ya ulevi wa pombe na sigara aliomba ushauri kwa dada yake huyo kabla na kujiunga na Jumuiya ya Islam Ahmadiyya kuwa, ataachana vipi na tabia zake hizo sugu za ulevi yeye akamueleza njia rahisi sana,Mwenyezi Mungu kisha tueleza tule vilivyo halali na safi,kwa hiyo akamueleza mfano hizo pombe mbadala wake kunywa visivyolevya kama vile soda na togwa lakini upande wa sigara alimueleza kila utavyohisi hamu kula jojo{bublish} hapa Napata picha kwa nini mzee Mubarak alikuwa anapenda sana togwa ,ushahidi tupewao na akina mama unasema mzee Mubarak siku aliyojiunga aliagiza pakiti zake zote za sigara na kuchoma moto hadharani, wake zake walipigwa na butwaa yeye aliwaeleza nitawambia kwa nini nimefanya hivyo.

Baadaye alipowaeleza wake zake walipinga kujiunga kwa sababu mzee mwenyewe alikuwa bado ajakomaa kwenye Jamaati kazi hii alimpa dada yake tena ya kuwahubiri wakeze bi mdogo alianza kujiunga na bi mkubwa akaendelea kuonesha upinzani lakini mwishoni mwaka huo baada ya njozi Fulani ambayo anaeleza ilikuwa ya kutisha sana na yenye uhusiano sana na upinzani wake njozi hii anapenda kuisimulia anasema haikuwa ya kawaida

MAISHA YA UDEREVA

Mzee Mubarak ni moja wa madereva wa muda sana waliolitumikia taifa katika fani hiyo hasa mara baada ya kupata uhuru, kama nilivyoeleza hapo udereva hasa alijifunzia mkoani Morogoro ambako anasimulia mwenyewe alikimbilia huko kwa watu baki kwa kujisalimisha kutokana na kutishiwa kuuawa na mtu Fulani kijijini kwao baada kumua mbuzi wake machungoni kama ilivyo desturi ya fujo za udogoni mzee Mubarak alipiganisha mbuzi wake na mbuzi wa bwana huyo alipoona mbuzi wake anazidiwa mzee Mubarak akachugua gongo na kumpiga Yule mbuzi wa mwanakijiji mwanzao Yule mwanakijiji akatangaza Mubarak lazima name nimuue hivyo alivyopata habari mzee Mubarak akaanza za kwa mguu na uzamiaji kwenye magari mpaka morogoro na alipofika huko akajifunza fani yaudereva

Mwaka 1954 sawa na taarifa aliyotupa alifanikisha kupata leseni yake ya kwanza class D na kuanzia hapo alianza kufanya kazi za watu binafsi na makampuni binafsi na miaka ya 1962 alifanya kazi katika sehemu mbalimbali za serikali na kilichofanywa awe na mvuto wa kuingia serikalini ni sifa zile za watu walikuwa wakimuita dereva mpole na makini, ndio mwaka 1962 akachukuliwa na serikali kuwa dereva wa utumishi wilaya ya songea,alieendelea mpaka miaka ya 1970 alipelekwa mkoani singida kumuendesha afsa maliasili wilaya ya manyoni mpaka mwaka 1974 ambapo alirudishwa mkoani Ruvuma kuwa dereva wa almashauri ya wilaya ya songea kitengo cha ushirika na ujamaa ambapo pia alipata barua ya kupandishwa hadhi kutoka dereva wa kawaida mpaka dereva wa daraja la nne

Endelea uk. 8

Bustani ya Washairi

AMETUITAIMAMU-WAPENDWATUBADILIKE

1. Ewe Uliye Mpweke, Ya Ilahi Ya Halimu
Nisemayo yashikike, yasipunguke utamu
Wasomaji wasichoke, isiishe yao hamu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

2. Wapendwa tubadilike, ametuita Imamu,
Mimbarini asikike, kukumbusha majukumu
Khalifa kilio chake, tusipoteze hatamu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

3. Kiongozi atutake, kwenye zake takalamu
Mwongozo wote tushike, ulotoka kwa Karimu
Kamwe tusikengeuke, amri kuzihujumu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

4. Katu tusidanganyike, hakuna ndogo haramu
Kila baya tuliruke, hilo ni sawa na sumu
Mema yote yatendeke, moja tusione gumu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

5. Malengo tuyakumbuke, ya sisi kuwemo humu
Na dhamirani tuweke, kuyafikia maqamu
Ya Masihi kuja kwake, Isa bin Maryamu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

6. Mapenzi yaongezeke, ya kumpenda Rahimu
Na imani isishuke, ichanue kwa kudumu
Ibada vyema tushike, Sala, Zaka na Saumu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

7. Kila mtu azinduke, kuishi kwenye nidhamu
Kisha tusiathirike, na wachonga masanamu

   Njia tusiichepuke, Lajna pia Khuddamu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

8. Kusoma kusipunguke, zikue zetu fahamu
Kwa pamoja tung'arike, tuwe mfano kaumu
Tulolala tuamke, kuihami Islamu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

9. Uchamungu tupambike, Mashekhe na waalimu
Kwa hofu tutemeke, ofisi kuzihudumu
Chema kigezo tuweke, watuigize kaumu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

10. Kwa dhati tuwajibike, yote yanotulazimu
Nyoyoni tuhalisike, utawa kila sehemu
Wito huu tuitike, Jamaat na Tandhiimu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

11. Mahubiri yatendeke, kwa hoja zenye elimu
Lakini mahala pake, khulka njema muhimu
Hapo ndipo yaitike, makundi kuja silimu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

12. Kwa mbali tuiepuke, tabia ya kulaumu
Khalifa naatamke, lake natuliheshimu
Tumuache peke yake, yule anayeshutumu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

13. Yabidi tuhuzunike, kuchezea yetu zamu
Kwa vilio tupasuke, kuifikiri hukumu
Mbele Yake tuanguke, Mwenyezi Atusalimu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

14. Ndugu vipi turidhike, hali zetu mahmumu
Iweje tughafilike, nasi si wendawazimu
Tusije tudhalilike, wenyewe kujidhulumu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

15. Naomba nikubalike, Mbeleyo Mola Adhimu
Wa kwanza nibadilike, nisimwangushe Imamu
Kisha waume na wake, tujali hizi salamu
Ametuita Imamu, wapendwa tubadilike.

Abdulrahman M. Ame
Dar.

VIPAJI VYA MPIRANI

1 Shairi ninaloimba, lenye vina na mizani
Nakusudia kulumba, soka la hapa nchini
Najitoma kwenye dimba, nikitoa tathmini
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

2 Kabumbu limefifia, halivutii machoni
Mafundi wa kupasia, nyavu hawapatikani
Wachezao hukimbia, kama wako zoezini
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

3 Vipaji tuliviunda, kwa wachezaji wa ndani
Likasakatwa kandanda, kwa umahiri wa fani
Leo wetu wamevunda, twakumbatia wageni
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

4 Hujing'ata kwa hasira, nikikumbuka zamani
Enzi za kina Manara, Sembuli na Kibadeni
Kimpira tuling'ara, na tulitisha barani
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

5 Makipa wenye kariba, walikuwapo mwanzoni
Na mabeki wa miraba, wenye nguvu maungoni
Viungo wenye kukaba, katika dimba la chini
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

6 Kulikuwa na mawinga, walosumbua pembeni
Wenye kasi ya kimbunga, ilotisha wapinzani
Na mafowadi kigaga, wenye shabaha golini
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

7 Eliasi na Mahadhi, wafananishwe na nani?
Au yupi mwenye hadhi, ya Mambosasa nchini?
Mlinda anayekidhi, mahitaji ya langoni
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

8 Mambo ya Tenga na Jella, yamebaki hadithini
Na ya Kajole Machela, kenda nayo kaburini
Hata ya Mwakalebela, leo hayaonekani
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

9 Watu kama yanga Bwanga, Mwaijibe na Thueni
Au Nico na Dilunga, ama Mwinda Ramadhani
Ni mahodari wa chenga, walokosa warithini
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

10 Wale Gaga na Mogella, asowakumbuka nani?
Kizota na Lunyamila, ni wa hivi karibuni
Wamekosa mbadala, soka limo ukiwani
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

11 Kila timu kwenye mji, ilifanya ushindani
Si Reli si Majimaji, na hata za mchangani
Hazikuwa uji uji, zikafungwa kilaini
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

12 Nguli wetu walitamba, nyumbani na ugenini
Na vichwa hawakuvimba, kwa sifa za mitaani
Licha ya mapato haba, hawakugoma kambini
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

13 Leo wanasoka wetu, hulipwa mamilioni
Hawakongi nyoyo zetu, waingiapo dimbani
Pasi na mashuti butu, havikupi burudani
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

14 Soka letu Tanzania, limeshapoteza shani
Wapenzi huzikimbia, mechi za hapa nyumbani
Na wengi wamehamia, soka la ughaibuni
Vipaji vya mpirani, nchini vimetoweka

Abdullah H. Mbanga (Kungwi)
Tambani – Mkuranga Pwani

NDOA BILA RAHMANI SI NDOA NI TAFRANI

1 Ndoa bila Rahmani, si ndoa ni tafrani
Ndoa isio imani, mwishoe ni hatiani
Haidumu asilani, hata ipambwe na nini
Ndoa bila Rahmani, si ndoa ni tafrani

2 Si ndoa bali utani, ukiichunguza ndani
Endapo utabaini, utalia kitandani
Siri kubwa ni imani, itulizayo moyoni
Ndoa bila Rahmani, si ndoa ni tafrani

3 Akiingia shetani, hapo huwa buriani
Hata awe Sultani, haponi bila Manani
Sio kama ninadhani, ukweli nilobaini
Ndoa bila Rahmani, si ndoa ni tafrani

4 Maneno yawe laini, ni bure bila Manani
Mlipo mpo gizani, nemazo hamzioni
Pambo jipambe mwilini, hishia duniani
Ndoa bila Rahmani, si ndoa ni tafrani

5 Msipokuwa makini, hamuishi mitihani
Tokeni usingizini, na Mola wenu mcheni
Jicho lililo gizani, hivi litaona nini?
Ndoa bila Rahmani, si ndoa ni tafrani

6 Kalamu naweka chini, kaditama niacheni
Muyaweke akilini, maneno ya muadhini
Kuishi bila ya dini, bora kuishi mwituni
Ndoa bila Rahmani, si ndoa ni tafrani

Issa H. Bunga
Kivule – Dar es Salaam

KUPOTEZA NI KUPATA

1. Matokeo ya susuri ni jambo lilo adhimu
Ikiwa mwisho ni shari surufi hiyo ni sumu
Iache ina hatari hususa kwa binadamu
Kupoteza ni kupata usihofu kupoteza

2. Mwisho wa kheri ni kheri, ni fitrati naimu
Kaumba Mola Kahari, kwa hatua na kwa zamu
Na hiyo ndiyo johari, Aliyopanga karimu
Kupoteza ni kupata usihofu kupoteza

3. Na sasa nakupa siri, jambo moja adinamu
Ukipoteza saghiri, pawe juu na kuzimu
Utaokota kizuri, kito kilo akramu
Kupoteza ni kupata usihofu kupoteza

4. Maisha kwenye sayari, hakika yana utamu
Ila kwenda kwa Satari, kuyapoteza muhimu
Na hiyo alaasiri, kwake mwana wa adamu
Kupoteza ni kupata usihofu kupoteza

5. Kupoteza ni uturi, hapa napiga hatamu
Nilosema tafakari, ya faida kw akaumu
Ni nzito hino habari, uliza wataalamu
Kupoteza ni kupata usihofu kupoteza

Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)
Dar es Salaam.

Ndoto 3 tukufu za Mtume Muhammad s.a.w

Ustadhi ***A .R. Mikila – Morogoro***

Kutoka toleo lililopita

NDOTO ZA MTUME MUHAMMAD (SAW).

Bila shaka tukio hili la watu kusujudu pamoja na Mtume Muhammad (saw) hadharani, na lile alililo shuhudia Sayida Umari mwenyewe kwa macho yake, la waislamu kuihama Makka kwa siri kukimbia bughudha zao, pamoja na mazingira mengine mengi, ndiyo yaliyo pelekea Sayidina Umari bin Khatwabu, baada ya muda mfupi tu kupita atangaze kusilimu.

07-Miraji iliutambulisha Uislamu Barani Afrika.
Muda mfupi tu, baada ya ndoto hii kupatikana, Uislamu ulipata mkondo wa kutiririsha maji ya Baraka ya mafundisho yake nje ya Makka. Mkondo wa mafundisho hayo ulifika barani Afrika kupitia Ethiopia. Kutoka Ethiopia uislamu uliweza kujulikana na kuenea sehemu kubwa ya Afrika. Hii ndiyo Mi'raji - mbingu za mafundisho ya Islam zilifunguka.Amni kwa Bara la Afrika.

08 - Miraji iliweka mizani ya Uchamungu wa kweli.

Uadilifu wa Mchamungu wa kweli, hujlikana wakati mtu huyo anapo takiwa kutoa maamuzi magumu na kutafuta njia sahihi ya kuihami dini anayo ihubiri, dhidi ya hatari ya kuipoteza kwa njia ya kupoteza maisha ya wafuasi wake.

Mtume (saw) aliliona hili, ndiyo maana alitoa uamuzi ule kwamba, ni vema baadhi ya waislamu waihame Makka waende nchi nyingine, kwa usalama wa dini na maisha yao. Njia hii bora na uamuzi huu mgumu, uliweza kuinusuru dini na wafuasi wake wengi.
Hii ni hekima kubwa ya kiucha mungu, ambayo ili iwezesha Islamu kama dini kunusurika katika maangamizi yaliyo kusudiwa na Makafiri kwa yale matendo yao ya kuwaua na kuwatesa waislamu kila kukicha. Mtume (saw) aliona kuwa haitakuwa busara, waislamu wote kuendelea kuishi katika mji mmoja, wenye maadui kila upande.

Kwa kuwagawa baadhi ya waislamu,na kuwataka wahame waende kuishi Ethiopia na wengine wabakie Makka, alionyesha hekima kubwa ya kuufanya uislamu uendelee kubaki hai, uendelee kukua na hatimaye kuenea hata nje ya Makka. Kwa hekima hii mbinu za Mtume (saw) zilishinda na mbinu za Wapinzani wake wa Makka zikashindwa.

Hizi ndizo zile salamu za amani ambazo Mtume (saw) alizo kuwa anapewa katika kila Mbingu aliyo ingia siku ile ya usiku wa Mi'raji.

09 – Mi'raji iligundua ardhi ya watu wema na Mtawala mwema.
Amani iwe juu ya Ethiopia na amani iwe juu ya Mfalme Najashi. Historia ya dini ya Islamu haikamiliki bila kuitaja nchi ya Ethiopia na bila kulitaja jina tukufu la Mfalme huyu.

10-Mi'raji iliweka mpangalio mzuri wa nyakati za sala za Jamaa.
Jambo hili halihitaji maelezo mengi. Sote leo ni mashahidi, tunazo adhana tano kila siku, kwa ajili ya sala za jamaa. Sala hizo ni zile alizo pewa Mtume (saw) usiku wa Mi'raji.
Qur'an inasema:-
"Usimamishe sala jua linapo pinduka, mpaka giza la usiku, na usome Qur'an Alfajiri. Hakika kusoma Qur'an Alfajiri kunakubalika sana" (17:79).
Baada ya Mi'raji Waislamu walianza kukutana kwa sala kutwa mara tano.

2.- SAFARI YA ISRA – KUTOKA MAKKA KWENDA MASJIDI AQSAA
Safari ya Isra ndiyo ya pili baada ya ile ya Mi'raji. Kindoto Mtume (saw) alisafiri kutoka Makka kwenda masjidi Aqsaa (Jerusalemu). Safari hii inajulikana kwa jina la **Isra** na ilifanyika katika mwaka wa kumi wa utume wake. Katika ndoto, Mtume (saw), alijiona anasafiri kuelekea kusikojulikana, lakini baadaye akajiona yupo **Baitul Muqadasi (Jerusalemu)**.
Ndoto hii aliiota katika kipindi ambacho yeye na wafuasi wake, pamoja na watu wa ukoo wake walikuwa ndiyo kwanza wametoka kifungoni kwenye lile bonde la Abu Twalibu, walikozuiwa kwa muda wa miaka mitatu wasitoke kuchanganyika na watu wengine wa Makka. Na katika siku hizo hizo Mtume (saw), akapatwa na misiba miwili adhimu. Msiba wa kwanza, ni kufiwa na mkewe kipenzi Bi Khadija (r.a), msiba wa pili ni kifo cha baba yake mdogo, mzee Abu Twalibu. Vifo hivi viwili vilifatana kwa kitambo kifupi tu cha mwezi mmoja. Kufatia misiba hiyo miwili, Mtume s.a.w, alihamia kwa binamu yake Umu Hani bint Abu Twalib, na kuishi kwake kwa muda. Ni katika kipindi hicho alipokuwa, nyumbani kwa Umu Hani, ndiko Mtume s.a.w, aliko ota ndoto hii ya **ya Isra**. Asubuhi yake alipo amka akamsimulia nduguye huyu ndoto hii.

Ndani ya ndoto hii, Mtume (saw), alijiona amesafiri kwenda Baitul Muqadasi na kurudi Makka. Safarini alijiona amempanda mnyama kwa jina la Buraku. Kiongozi wa safari kama kawaida, alikuwa Malaika Jibrili. Masimulizi ya safari hii ya ***Isara*** ni marefu, na yame jaa nakshi nyingi. Kwa sababu ya nakshi hizo, ndiyo maana waislamu wa baadaye waligawanyika makundi makundi, katika kuifahamu hakika yake.


Ustadh Abdulrahman Mikila

Wapo wanao simulia **safari ya Isra na Miraji** kwa kuziunganisha na kuzifanya safari hizo mbili kuwa moja, yenye sehemu mbili. Kundi hili lina amini kwamba safari hizo zilikuwa ni za kimwili halisi. Wao wanazigawa safari hizo katika sehemu mbili. Kwanza ni ile safari ya kutoka Makka kwenda Jerusalemu, pili ni ile safari ya kutoka Jerusalemu kwenda mbinguni.
Kundi la pili ni la wale wasemao, **Safari ya Isra** haifungamani na **safari ya Miraji**. Kila safari ilifanyika kwa wakati wake na kwa miaka tofauti. Bali safari zote hizi mbili,wanasema zilikuwa safari halisi za kimwili.

Kundi la tatu ni sisi Waislamu wa ahmadiya na baadhi ndogo sana ya waislamu wengine; sisi tuna amini na kuthibitisha kwamba, safari ya Mi'raji na safari ya Isra, zote hizo zilikuwa si safari halisi za kimwili, bali zilikuwa ni safari za kindoto na kila moja, ilifanyika kwa wakati wake na kwa mwaka wake. Tunaamini hivyo, kutokana na ushahidi mpana wa Qur'an Tukufu juu ya safari hizo, pia ushahidi wakimazingira wa viashiria vya ndoto vinavyo patikana katika matukio ya safari hizo. Kadhalika ushahidi wa historia ya Maisha yake Mtume (saw), hauonyeshi kwamba, aliwahi kufika Jerusalemu wakati wa uhai wake.
Msomaji wangu mpendwa ni vizuri uitalii Qur'an Tukufu kwa kina juu ya safari hizi za kimiujiza. Pia fanya udadisi wa masimulizi ya safari hizi, na yaliyomo ndani ya vitabu vya hadithi za Mtume (saw). Pia pata wakati wa kutafakari matukio makuu yenye taathira katika maisha ya Mtume Muhammad (saw). Naamini nyenzo hizo zitakusaidia kupima hoja zetu na ushahidi unaotolewa na Qur'an Tukufu pamoja na hadithi hizo. Vile vile jaribu kuainisha ufahamu wako juu ya historia ya Maisha yaMtutume Muhammad (saw) na masimulizi hayo. Bila shaka utagundua kuwa kundi hili linazo hoja madhubuti na zenye mashiko na zinazo kubalika kiakili.

USHAHIDI WA Qur'an TUKUFU
Ndani ya Qur'an tukufu safari hizo zimetajwa katika sura mbili tofauti. Sura ya 53, An-Najimu na Sura ya 17, Banii Israil. Sura An-Najim, ilishuka Makka katika mwaka wa 5 wa utume, humo imetajwa **Safari ya Mi'raji**. Sura ya Banii Isaraeli, ilishuka Makka mwaka wa 10, humo imetajwa-**Safari ya Isra**.

Sura hizi mbili, ziliteremshwa katika nyakati tofauti na kwa madhumuni tofauti. Kisha zimepishana kwa umbali wa miaka mitano kati ya sura moja na nyingine. Safari ya Mi'raji ndiyo ilikuwa ya kwanza, ilifanyika mwaka 5 wa utume wake. Wakati huo hali ya uadui na uhasama dhidi ya waislamu ilipata sura ya utaifa ya muungano wa maadui.
Baadaya Mi'raji ikafatia Safari ya Isra, katika mwaka wa 10 wa utume wake. Safari hii ilitokea baada ya yale madhila ya kuwekewa vikwazo na maadui zao vya kiuchimi, kijamii na huduma za kiutu na kutengwa na kunyimwa mawasiliano yote muhimu kwa muda wa miaka mitatu.

Kwa mtiririko huo wa safari na mazingira yake, ni dhahiri kwamba si sahihi, kusimulia safari hizi mbili kwa kuziunganisha na kuzifanya kuwa moja na zenye kufatana. Pia si sawa kuitanguliza safari ya Isra kuifanya kuwa ya kwanza na Mi'raji kuwa ya pili.

MWANZO WA SAFARI YA I SRA
Hebu tuyachunguze baadhi ya matukio katika masimulizi ya **safari hii ya Isra**. Kisha tuone hali ya msafiri huyu ilivyo kuwa usiku ule.
Safari ya Isra ilianza usiku wa manane. Mtume (saw), aliona mambo mengi njiani, na mengi yalimshangaza. Hata nasi tusomao leo kisa hiki yanatushangaza zaidi.

Mtume (saw), anasema alipitishwa katika nchi ya yenye Mitende mingi, akapitishwa katika Milima ya Sinai na hatimaye katika mji wa Baitul Lahamu (Betelhem), akiwa amepanda mnyama asiye mfahamu kabisa. Mnyama anayeruka na kuchupa gizani bila mbawa. Kote alikopitishwa aliamrishwa na Malaika Jibril a.s, kusali katika kila kituo kikuu cha sehemu hizo. *Bila shaka sala hizo zilikuwa za Nafal*.
Pia Mtume (saw), anasimulia kwamba, mwanzoni tu wa safari; kabla hata hawajaenda mbali, akamuona mwanamke ajuza amesimama kando ya barabara, ameshika kijinga cha moto anamfata yeye, hapo Malaika Jibrili akamfundisha dua ya kusoma dhidi ya tukio lile. Safari iliendelea mbele, hata wakafika nchi fulani, akawaona watu wake wanalima siku moja na kuvuna siku ya pili yake. Hapo mtume s.a.w, akamuuliza Malaika Jibril hali hii, maana yake nini? Jibril akajibu, Maana yake ni kwamba, hawa ndiyo wale watu wanao pigana kwa ajili ya dini ya Allah, hupewa thawabu zao mara mia saba na kuzidishiwa zaidi. *Lakujiuliza hapa ni hili, nchi gani hiyo, inapatikana wapi katika ramani ya dunia? Muda wa kuona yote hayo uliupata wapi wa kuona yote hayo?Tafakari.*

Kwa kifupi safari nzima ya **Isra** ilijaa matukio ya ajabu na ya kushangaza ya namna hii.

Mengi katika matukio hayo yalikuwa yapo kinyuma na ufahamu wa kawaida. Hali hii isiyo ya kawaida, ndiyo iliyo mlazimisha Mtume (saw), mara kwa mara kuuliza uliza kwa Malaika Jibril a.s, ili apewe maana ya matukio yale. *Hapa inaonyesha wazi kuwa Mtume (saw) hakuwa katika hali yake ya ya kawaida ya utashi na ufahamu.*
Hatimaye Mtume (saw), na Malaika jibril (as) wakafika Baitul Muqadasi. Waliwakuta Mitume wa zamani wakisubiri kumlaki Mtume (saw). Baada ya hapo, ikanadiwa sala, Mitume wote wakasali sala ya jamaa nyuma ya Mtume (saw). *Haikutajwa sala hii ni tahajudi* au *sala ya Alfajiri.Tafakari.* Pia imeelezwa kwamba walipofika Baitul Muqadasi, Malaika Jibril alimpelekea Mtume s.a.w, bilauri tatu za vinywaji. Bilauri moja ilikuwa ina maji ya kunywa, ya pili ina maziwa na ya tatu ilikuwa ina pombe. Mtume (saw), alichagua bilauri ya maziwa, akaichukuwa akanywa na kuziacha zile zingine. Malaika Jibril alimsifu kwa chaguo lake lile. *Katika hali ya kawaida Malaika Jibril asinge weza kumletea Mtume s.a.w, kinywaji cha pombe huku akijua ni haramu. Tafakari*. Je, msomaji wangu, mpaka hapo bado hujapambanukiwa? Nina amini umepambanukiwa na kwamba, sasa umepata mwanga na uwezo wa kutafakari vizuri safari hii ya **Isra** na matukio yake yote. Mwanga huo uliyo upata, basi uutumie kukuwezeshe kujua hakika ya safari hii ya **Isra** vile ilivyokuwa.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Mtaheshimika kwa matendo sio maneno

Kutoka uk. 4

kubwa zaidi, kwamba kama wao, yaani wabashiri na maulamaa, wafanye juhudi za kusafisha mioyo (ya watu) na kujaribu kuzalisha (mioyoni mwao), maarifa na mapenzi ya Mwenyezi Mungu, basi mamillioni ya watu wataanza kujiunga na Jumuiyya ya Waislamu Waahmadiyya, Allah Taalah Mwenyewe Anasema: Ufikapo msaada wa Allah na ushindi na kuwaona watu wakiingia katika dini ya Allah kwa makundi, basi mtukuze Mola wako kwa sifaze na umuombe msamaha, hakika Yeye ni Apokeaye sana toba. (110: 2-4).

Kwamba kama mtaeneza dini yenu kwa mahubiri basi mtu mmoja mmoja au wawili wawili watajiunga nanyi, lakini kama mtamtukuza Mwenyezi Mungu na kufanya istighfar (kuomba msamaha wa madhambi) na kuyafuta madhambi ya wanajamaati yenu, basi makundi na makundi ya watu wataingia katika dini na kujiunga nanyi.

Na mbashiri wetu aliyeniandikia kuwa sisi tulikuwa tunawashinda vibaya wapinzani wetu, aelewe kuwa lengo letu halitapatikana kwa kuwashinda vibaya wapinzani, bali litapatikana tu kwa sababu ya marekebisho ya vitendo hivyo. Basi muelekee kwenye mabadiliko yenu ya vitendo na mjitahidi kuwa wasaidizi na manaibu wa ukhalifa.

Hatuwezi kujishughulisha na mihadhara ya kielimu kwa miaka na miaka, kwani kama tunataka kupata maendeleo ya Jumuiya, na inshaallah Taala tutapata maendeleo, basi tunapaswa kushika njia zingine pia, nazo ni mabadiliko ya vitendo. Hivyo tunalazimika kuboresha matendo yetu, tunahitajika kukuza viwango vyetu vya uaminifu na vya amana, tunapaswa kushika njia halali za mapato yetu, sio kwa ajili ya kiasi fulani cha fedha tuidanganye halmashauri na kuuharibu ubora wa ukweli wetu na ubora wa kupata manufaa yetu.

Au kwa ajili ya kupata fedha tufungue kesi za uwongo. Tunapaswa kutekeleza shuguli zetu tunazopewa, kwa juhudi za kila namna na kwa uaminifu tu, kama tutafanya hivyo basi tutafunguliwa pia milango ya dunia pamoja na milango ya dini. Hii ni fadhili ya Allah kuwa jumuiyya, kwa jumla, ina athari nzuri kwa wengine. Lakini kama tutaiharibu imani yetu na uaminifu wetu kwa ajili ya manufaa madogo madogo ya dunia, basi yeyote atakaye fanya hivyo atachafua jina la Jmuiya.

Jinsi wabashiri wanapaswa kuwahimizia wanajumuiyya, vivyo hivyo kila mwanajumuiyya pia anatakiwa kujichunguza na kujipima kwa ajili ya kujirekebisha, na pamoja na hayo, silaha kubwa zaidi ni ya dua inayotakiwa kuzingatiwa muda wote na kuitumia vizuri. Na kwa ajili ya kufaidika vyema na silaha hii, tuzingatie amri hii ya Mwenyezi Mungu kuwa mjiongeze katika imani na mfuate desturi ile niliyoweka mbele yenu kwa ajili ya kutenda vitendo vizuri. Basi vitendo hivi vizuri na dua, au maombi na vitendo vikiafikiana vitaleta mabadiliko mazuri. Mwenyezi Mungu atuwezeshe sisi sote kuyatekeleza haya yote.

Mwishowe ningependa kuwaelekezeni kwenye jambo ambalo limemjeruhi kila mwislamu wa kweli, nalo ni hali halisi ya leo ya nchi za waaislamu. Umma wa waislamu unahitaji sana siku hizi, maombi ya wafuasi wa mpenzi wa kweli wa mtume Muhammad s.a.w., hivyo tunalazimika kufanya maombi kwa ajili yao.

Hali ya Syria inaendelea kuwa mbaya zaidi, utawala wao umesharuka mipaka katika kuwadhalumu wananchi na wapinzani wa serikali pia wanaruka mipaka katika kufanya dhulma, watoto, wazee na wanawake pia wanadhulumiwa. Wanawakamata watoto na wanawake na kuwaweka ndani kwa njaa, hata kama hana kosa lolote, kisha wanateswa, picha za baadhi yao zimeoneshwa kwenye tv. na mwili wote unasisimka kwa kuzitazama zile picha, kwani mwislamu anamdhulumu mwislamu mwezake kwa kiasi hiki na anawapa nafasi maadui wa kuleta upinzani dhidi ya uislam.

Wamerusha hewani mahojiano ya baadhi ya vijana wenye umri wa miaka 14 au 15, ambao wamesha poteza wazazi wao au kutengana nao kwa sababu moja au nyingine, ambao huhangaika kwa ajili ya chakula na hawapati cho chote cha kula, na mmoja wao, mwenye umri wa miaka 12 au 13, alipoulizwa na mwenye kufanya mahojiano kuwa utafanya nini utakapo kuwa mkubwa, basi alimjibu kwamba ni wazi nitakuwa mhalifu, mwizi, janbazi na gaidi, ili tuweze kujilipia kisasi.

Wanaendelea kuharibu kizazi, wenye mamlaka kwa ajili ya kuyalinda mamlaka yao, na wapinzani kwa ajili ya kuupata utawala. Mwenyezi Mungu Awafikishe hawa wadhalimu kwenye malipo yao, na awalinde watu na dhulma yao na kuleta mahakimu waadilifu. Dhuluma inazidi kuongezeka huko Pakistan pia, hususan dhidi ya waahmadiyya, ambao wanaudhiwa kiroho na kimwili pia. Hata wananchi wa kwaida wa Pakistan pia wanaendelea kudhulumiwa, na inaonekana dhulma na mateso yataendelea kuzidi, makundi mbali mbali ya wadhalimu wanasaidiwa na wenye mamlaka, hivyo kuwadhibiti pia inakuwa ni vigumu. Basi dua ni silaha ya pekee inayoweza kuwashika hawa wadhalimu, maombi mengi yanahitajika ili Mwenyezi Mungu Awamalize wadhalimu hawa kutoka Pakistani na halikadhalika nchi zingine za waislamu kama Libya, Misri na kadhalika, na hali ni mbaya mno katika kila nchi. Mwenyezi Mungu Awape akili na Ailinde Islamu na harakati zao duni zinazoichafua Islam. Mwenyezi Mungu Awafanye hawa wadhalimu ishara ya onyo, na Allah Taalah Amlinde kila muahmadiyya anayeishi katika nchi hizi.

Wasifu wa Marehemu Mzee Mubarak Athumani

Kutoka uk. 5

liloambatana na mabaliko ya kiwango cha mshahara,mwaka 1980 aliteuliwa kuwa dereva wa mganga mkuu wa hospitali ya mkoa wa Ruvuma na miaka 1990 alipumzika kwa kuachana kabisa na kazi hiyo ya udereva isipokuwa kwa sababu ya uzee ambapo aliona kazi hizo amechoka,isipokuwa miaka ya 1994 aliombwa na awe dereva wa jamaati ,mzee kwa moyo mkunjufu alikubali , nakumbuka akiwa songea kwa nyakati tofauti aliwaendesha masheikh wetu mbalimbali akianza na maulana sheikh Bakri Amri Abeid,baadaye sheikh Fareed Tabasamu,na kumalizia na maulana Sheikh Abdul Nasir,ndipo jamaati ikamuamisha kuwa dereva wa jamaati mkoani Iringa kisha Morogoro na baadae kumalizia Tanga ambapo sawa na umri alishauriwa apumzike

AWA MLINZI WA MSIKITI WA JAMAATI SONGEA

Baada kifo cha marehemu mzee Athumani Ndembo Ahmadiyya ambaye alilinda msikiti wa songea (masjid furqan) kwa miaka mingi kidogo jamaati ya songea ilipata taabu kidogo kumpata mlinzi mwingine lakini mzee Mubarak pamoja na umri mkubwa alivyopata tu taarifa akiwa kijjini mageuzi alisema wacha hii kazi niifanye mimi japo alishauriwa na akina mama na watoto sawa na umri wake asifanye ambapo wale si Ahmadiyya wakaenda mbali na kusema kama anashida yoyote ni kheri aseme kuliko kufanya kazi hiyo ambayo ni hatari kwa umri wake lakini mzee Mubarak jibu lilikuwa acheni nikafanye kazi hii yenye faida zaidi kwani sifanyi kwa sababu ya malipo hayo kidogo bali kuna shida ya kupatikana mlinzi

TUNALO LA KUJIFUNZA KABLA YA VIFO VYA WAZEE HAWA WAWILI

Kumbukumbu yangu inanirejesha siku ambayo mzee mubarak siku chache kabla idd el fitri alikuja hapa Dar-es salaam kwa ajili ya kujipumzisha kwa vijana wake na kuchunguza afya yake nilionana na marehemu mzee wetu mpendwa Ndugu Ahmad Fransis hapa masjid salaam , na kumueleza mzee Mubarak amefika dar kwa ajili ya matatizo ya afya nakumbuka mzee Fransisi alinieleza inshallah ataonana naye kwenye idd na kama atashindwa alinieleza kuja basi yeye mzee fransis nimpeleke pale alipofikia mzee Mubarak, bahati nzuri siku ya iddi mzee Mubarak alishiriki sala iddi ambapo alikuja kitonga kwa msaada wa kijana wake, siku hiyo walikusanyika wazee wangi wa kijamaati akiwemo mzee fransi, sultani ungando na wengineo wakiriwadha kwa habari za nyuma kuhusu jamaati yetu, yaonekana kwamba shauku na hamu ya kuonana yao mzee mubaraka na fransis bali mzee Mubarak siku chache baada ya iddi alimfuta mzee fransis pale masjid salaam ambapo wakati anamsindikizajioni mzee fransis wengi wetu tunajua masihibu yaliyomkuta marehemu mzee fransis,kitu tunachojfunza kwa wazee hawa ni kiwango cha juu cha mapenzi miongoni mwao ambayo masihi aliyoahidiwa aliyataka tuyafikie

ACHANGIA MCHANGO WA UKOMBOZI BARA LA AFRIKA

Kilichonifurahisha pia umahiri wake mzee Mubarak wa utunzaji kumbukumbu zake muhimu zile za maisha yake ya kikazi na jamaati ukweli huu umejidhirisha wakati tukipekua nyaraka zake tukizikuta nyaraka za tangu mwaka 1960 au zaidi ya hapo mfano barua yake yakuombewa ruhusa na mbashiri wa mkoa kwa mkubwa wake wa kazi kuwa mjumbe wa jamati mkutano wa mtama mwaka 1977,lakini jambo lilonifurahisha ni lille la uzalendo kwa bara la afrika ambalo azimio lake pia lilitangazwa na mwalimu nyerere mara baada ya kupata uhuru kwamba uhuru wetu hautaweza kuitwa kamili mpaka tuone nchi zote za Afrika ziko huru ,alisema Tanzania imo kati ya nchi chache ambazo zimetanguliwa inadhamana kubwa juu ya hilo akiwaomba hasa wafanyakazi ambao wanakipato angalau kinachoeleweka na cha uhakika,naye mzee Mubarak akuwa nyuma juu ya hilo , kwani kutokana na ushaidi wa kinyaraka tumekuta moja ya risiti ambapo alichangia mchango huo mwaka 1974 fedha aliyochangia ilikuwa ni shilingi kumi na senti themanini.

Sisi sote ni wa mungu na kwake tutarejea

= Mwisho=

Wasifu wa Maulana Sheikh Abdulkarim Sharma

Na Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya – Songea

Kutoka toleo lililopita

Alipokuwa katika kituo cha Tabora alifanya juhudi ya kusomesha vijana wa Kiahmadiyya na kuwakusanya katika kituo hicho hicho cha Jamaat. Hatimaye vijana wawili walipelekwa Pakistan kwa masomo ya juu ya dini ambapo kijana mmoja Bw. Ali Swalehe alishindwa njiani ila kijana wa pili Bw. Yusuf A. Kambaulaya alirejea nyumbani baada ya kupata mafanikio.

Ikumbukwe kuwa Sheikh Sharma aliwahi kuwa Mubashiri Mkuu na Amir nchini Uganda pia. Alipokuwa Nyanza Kisumu walishirikiana na marehemu Sheikh Munawwar kuhubiri dini ya Kiislam na kuwalea waliojiunga na Uislam kwa juhudi za Masheikh wa Kiahmadiyya. Huko Luanda alifanya kazi ya kuwasilimisha Wakristo wengi wakauhama Ukristo. Huko Yunguli alipambana Padre mmoja aliyedaiwa kupokea ufunuo wa Mungu, lakini Padre alishindwa kuthibitisha madai yake mbele ya Sheikh Sharma. Mwaka 1978 alistaafu rasmi na akawa anaishi huko Uingereza. Alifanya kazi akiwa Katibu wa Tabligh, Mjumbe wa Majlis Amila kwa miaka 10 pia akateuliwa kuwa Mjumbe wa pia akateuliwa kuwa Mjumbe wa maadhimisho ya sherehe za karne Uingereza.

Mwenyezi Mungu Aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amin.

= Mwisho=

Sheria za Mahakama ya Qadhi sio za Kiislam, Biblia ni jibu acheni kupotosha watu

Na Mwalimu Kais Ali wa Mkongotema, Madaba Songea

Hivi sasa Taifa letu la Tanzania lipo kwenye mchakato wa kihistoria wa kupata katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, taasisi mbalimbali pamoja na wananchi wapo kwenye kazi kubwa ya kujadili rasimu ya katiba. Lakini pamoja na serikali yetu kutoa ruhusa kwa taasisi na wananchi kuijadili rasimu hiyo kumetokea na mabishano makubwa kati ya baadhi ya waumini wa dini ya Kikristo na Waislam kuhusiana na suala la baadhi ya Waislamu kuitaka serikali iweke kwenye rasimu ya katiba kipengere cha mahakama ya Qadhi na cheo cha Qadhi kwa Waislam, jambo ambalo waumini wa dini ya Kikristo wanalipinga kwanguvu zao zote. Mimi mwenyewe mwandishi wa makala hii nimeshuhudia nikiona viongozi wa Kikristo wakiendesha semina kwa waumini wao hapa Mkongotema na Madaba (Songea), wakiwaeleza waumini wao wapinge suala la kuwepo kwa kipengere cha mahakama ya Qadhi katika katiba kwa sababu eti sheria za Kiislamu ni za kikatili na zinakiuka mipaka ya haki za kibinadamu.

Taasisi ya kidini inayojiita Biblia ni jibu kwa muda mrefu imejifanya kuchukua dhamana ya kuwaelimisha waumini wao Wakristo kuhusiana na mambo ya dini ya Kiislam ingawa kwa hakika watu hawa Biblia ni Jibu hawana elimu kabisa ya mambo ya dini hasa dini tukufu ya Kiislam, hivyo watu hawa Biblia ni Jibu kwa kuwa hawana elimu ya dini ya Kiislam au kutokana na uadui na upinzani waliokuwa nao dhidi ya dini ya Kiislam wamejikuta wakati wote wanapotaka kutoa maelezo yao yanayohusu dini ya Kiislamu wamekuwa wakiwapotosha watu wakati wanafahamu ukweli wa mambo. Kwa mfano hivi sasa watu hawa

Biblia ni Jibu wamesha andika machapisho yao mbalimbali ya vitabu na vipeperushi wakielezea na kuiomba serikali pamoja na Wakristo wote nchini wasikubali kuundwa kwa mahakama ya Qadhi kwa kuwa sheria za Kiislamu zikiwekwa kwenye katiba zitawanyanyasa Wakristo, na watu wa dini zingine. Ingawa katika makala yangu hii sipendi kabisa kuzungumzia mjadala wa upatikanaji wa mahakama au kuwepo kwa Qadhi, kwa sababu hoja hiyo ya kuwepo kwa Qadhi na mahakama ya Qadhi ni hoja iliyopitwa na



Mwalimu Kais Ali

wakati, hivyo hoja hiyo sasa haina mashiko kwa sababu Waislam duniani kote tatizo linalowakabili sio kuwepo kwa Maqadhi au Mahakama ya Qadhi, bali Waislam hivi sasa duniani kote wanayo matatizo makubwa ya kupata mwongozo na mafundisho safi ya kiroho hivyo anatakiwa apatikane kiongozi mkubwa wa kidini atakayeweza kutibu maradhi hayoya kiroho. "QADHI" Ni neno la kiarabu na maana yake ni (a) "Al-Sultwan" yaani mtawala (b) "Al-Hakim" yaani Hakimu. Hivyo basi Waislamu wanapodai kuwa awepo Qadhi wanamaanisha awepo mtawala na hakimu atakayewaongoza Waislamu katika masuala yao ya kidini.

Katika zama hizi tulizo nazo ilisemwa ni zama za upotevu na maovu mengi sana ilitabiriwa katika dini zote kuwa maovu yatakapojaa duniani Mwenyezi Mungu Atamtuma Mtumishi wake yaani Nabii wa Mwenyezi Mungu atakayekuja kufanya kazi kubwa sana ya kuwarudisha wanadamu wote kwenye mafundisho sahihi ya Mwenyezi Mungu yaani mafundisho ya Kurani Tukufu kitabu ambacho ni maneno matakatifu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Waislam waliambiwa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kuwa; "YUUSHIKUMAN AASHA MIN KUMAN'YALKA ISA BUN MARIAMA IMAMAN MAHDIYYA HAKAMAN ADLAN". Tafsiri – Ni karibu atakayekuwa hai miongoni mwenu akutane na Isa bin Mariamu akiwa Imamu Mahdi na Mwamuzi (Hakimu) mwadiifu. (Musnad Ahmad bin Hambal Jal. 2, Uk.411). Katika hadithi hiyo hapo juu ni dhahiri kuwa kuja kwa Nabii Isa mara ya pili ndiye atakayekuwa Hakimu na Mwamuzi Mwadilifu. Hapana shaka huyo Hakimu mwamuzi Mwadilifu ambaye pia ni Nabii wa Mwenyezi Isa mwana wa Mariamu aliyekuja kwa namna ya mfano wa Isa wa mara ya kwanza ameshafika tayari ni Mwanzilishi mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya, yaani ni Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) kwa mantiki hiyo kwa kuwa yeye ametumwa na Mwenyezi Mungu basi hivi sasa kibali cha mtu kuwa kiongozi wa kuongoza Waislamu mahala popote duniani kibali hicho kinatoka katika Jumuiyya yake aliyoianzisha kwa amri ya Mwenyezi Mungu hivyo basi hivi leo Waislam wanatakiwa wafahamu kuwa Maqadhi wa ukweli waadilifu watatokana na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Kinyume chake mtawapata Maqadhi makanjanja, magumashi ambao hawana uwezo wala elimu ya kuwaongoza Waislam. Bali tama yao itakuwa ni mali na kugombea madaraka kama tuonavyo hivi sasa kwa Waislam. Kwa mantiki hiyo ninawaomba ndugu zangu Waislam wasiendelee kupoteza muda bure kwa hoja ya kuwepo kwa mahakama ya Qadhi, hoja ambayo hivi sasa haina msingi. Waislam wajaribu kuangalia walipojikwaa wasiangalie mbele walitokoangukia. Walipojikwaa ni pale wanapojifanya kuwa vipofu kwa kutoona macho ya kiroho na kujifanya hawasikii kumbe wanasikia kwa kutotambua utabiri wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kuhusiana na ujaji wa mara ya pili kwa Isa Mwana wa Mariam atakayekuwa kiongozi mkuu kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambaye ni Hakimu Mwamuzi Mwadilifu, kwa kosa hilo wanaloendelea kulifanya Waislam la kutomtambua Nabii wa Mwenyezi Mungu aliyetumwa katika zama hizi sawa na utabiri wa Mwenyezi Mungu utabiri wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw), Waislam leo duniani kote wamejikuta ni watu waliodhalilika, kila aina ya madhila hivi leo yapo kwa Waislam kwa mfano leo katika elimu Waislam wapo nyuma sana, katika mambo ya uchumi pia wapo nyuma sana, Waislam duniani ndio wanaoonekana katika jamii ni waletaji wa vurugu na vita, katika nchi za Ulaya ukiwaacha Waislam wa Ahmadiyya wanaofuata mafundisho safi ya Islam, Waislam wanaobakia wanaonekana ni magaidi. Sasa matatizo haya yote yanayopatikana kwa Waislam yanatokana na kupuuza utabili wa Mtume Muhammad (saw).

Pia Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema katika Kurani Tukufu kwamba; "Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu (Waislam) na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya Makhalifa (Viongozi) katika ardhi kama Alivyowafanya wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimarishia dini yao (ya Kiislam) Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu hawatanishirikisha na chochote na atakayekufuru (atakayekataa Ukhalifa) baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri (za Mwenyezi Mungu". (Kurani Tukufu 24:56)

Na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alisema kwamba; "Imesimuliwa na Hadhrat Hudhaifa (ra) ya kwamba Mjumbe wa Allah (asw) alisema; 'Unabii utakuwa baina yenu mpaka apendapo Allah, kisha atauondoa, kisha utakuwepo Ukhalifa juu ya njia ya Unabii mpaka Allah akipenda uwepo, kisha atauondoa pia, kisha utapatikana ufalme wa kuudhi ambao utakuwa mpaka Allah atakapopenda kuwepo. Kisha Allah atauondoa, kisha utapatikana ufalme wa kimabavu na utaendelea mpaka Allah akipenda uwepo, kisha atauondoa, kisha utapatikana Ukhalifa juu ya misingi ya Unabii. Kisha Mtume (saw) akanyamaza'. (Musnad Ahmad, Mishkaat)".

Tena Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alisema kwamba; "Imesimuliwa na Hadhrat Safina (ra) ya kwamba yeye alimsikia Mjumbe wa Allah (saw) akisema; 'Ukhalifa utakuwa kwa miaka thelathini, kisha baadae ufalme utapatikana. Bwana Safina akasema; Haya hesabuni sasa. Ukhalifa wa Abubakar (ra) miaka miwili, Ukhalifa wa Seyidna Umar (ra) miaka kumi, Ukhalifa wa Uthman (ra) miaka kumi na miwili, na Ukhalifa wa Ali (ra) miaka sita. (Musnad Ahmad)".

Kwa mantiki hiyo sawa na aya ya Kurani Tukufu pamoja na Hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad (saw) hapo juu kilichotabiriwa kufika baada ya Mtume Muhammad (saw) kuondoka ni Uongozi wa Ukhalifa utakaopatikana katika misingi ya Unabii, kwa hiyo kwa ndugu zangu Waislam wafahamu kuwa nafasi ya kuchaguliwa Maqadhi hivi sasa haipo, bali hivi sasa yupo Khalifa ambaye pia ni Nabii aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu moja kwa moja ambaye sio mwingine bali ni Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) ambaye pia ni Masihi wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) aliyetabiriwa kuja katika zama hizi za upotevu kwa Waislam na wanadamu wote duniani. Na baada ya kufariki kwake Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) Ukhalifa uliotabiriwa na Mwenyezi Mungu katika Kurani Tukufu sura ya 24:56 ukawa umerejea tena kwa Waislam wa Ahmadiyya, hivi sasa tunaye Khalifa wa tano Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) ambaye anawaongoza wa Ahmadiyya wote kote duniani. Na Jumuiyya ya Ahmadiyya inaendelea kupata mafanikio makubwa sana hasa hasa katika nchi za Ulaya ambapo Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya imejenga misikiti mingi na nyumba za watumishi wa Jumuiyya ya Ahmadiyya.

Kwa ndugu zetu Wakristo kuhusu uongozi wa Ukhalifa pia imesemwa katika Biblia kwamba, "Wakati wa wafalme hao, Mungu wa mbinguni ataanzisha ufalme (uongozi wa kiroho) ambao kamwe hautaangamizwa, watu wengine hautaushinda na kuutawala ufalme huo, bali ufalme huo utaziponda na kuzikomesha falme zilizotangulia, nao utadumu milele". (Danieli – 2:44).

Sawa na utabiri huo hapo juu wa Biblia kuhusu uongozi wa Ukhalifa, imetabiriwa kuwa neema hii ya uongozi wa Ukhalifa ambao ni wa kidini hakuna mtu yeyote atakayekuwa na uwezo wa kuufuta na utadumu mpaka siku ya mwisho ya kiyama, kwani Mwenyezi Mungu Mwenyewe ndiye Atakayetoa ulinzi wake kwa ajili ya uongozi huo wa Ukhalifa. Na ndivyo ilivyokuwa katika Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya viongozi wake yaani Makhalifa wote watukufu wamelindwa na Mwenyezi Mungu ingawa maadui wa Jumuiyya hii wanahaha mpaka sasa ili kutaka kuiangamiza Jumuiyya ya Ahmadiyya lakini mpaka leo wameshindwa wamebakia midomo wazi, wamepigwa na bumbuwazi wanaiona Jumuiyya ya Ahmadiyya inazidi kusonga mbele inapata maendeleo makubwa sana duniani kote kwa mfano tarehe 26/04/1984 Serikali ya Pakistani ilipitisha sheria ya kidhalimu ikatangaza kuwa wa Ahmadiyya sio Waislam na wala haifai wenyewe wa Ahmadiyya wajiite Waislam, kusudio lao kubwa ilikuwa

Endelea uk. 10

Sheria za Mahakama ya Qadhi sio za Kiislam,

Kutoka uk. 9

ni kutaka kumkamata Khalifa wetu wan ne Hadhrat Mirza Tahir Ahmad (rh) wamfungulie mashtaka ya uongo ya uhaini halafu baadaye watake kumnyonga (Fanaudhubillah mindhaalika) wakiamini kuwa kufanya hivyo itakuwa tayari Jumuiyya ya Ahmadiyya itasambaratika duniani kote, Rais wa Pakistan wa wakati huo (Bw. Zia-ul-Haq) akatangaza nchi nzima kuwa mahala popote atakapoonekana kiongozi wa Ahmadiyya Mirza Nassir Ahmad akamatwe, ulikuwa ni mpango wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kumwokoa Khalifa wake katika mikono ya wahuni akina (Zia-ul-Haq) badala ya kusema akamatwe Mirza Tahir Ahmad tangazo la Zia-ul-Haq likasema akamatwe Mirza Nassir Ahmad angalia jinsi mipango ya Mwenyezi Mungu inavyopindua hila za makafiri na wapinzani wa Mwenyezi Mungu. Kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Kurani Tukufu kwamba; "Bila shaka sisi tunawanusuru mitume wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi" (40:52). Kama ilivyokuwa kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) siku alipohama Makka kwenda Madina makafiri wa Makka waliizunguka nyumba yake usiku wakitaka asubuhi ya Alfajiri atakapotoka ndani wamkamate ili wamwue, lakini asubuhi ilipofika alitoka mule ndani na kuwapita pale mlangoni bila kumwona ingawa pale mlangoni waliweka ulinzi wa askari wa kulinda lakini alifanikiwa kuwaponyoka akaenda uhamishoni katika nchi ya Madina.

Ndivyo ilivyotokea kwa kiongozi wa Jumuiyya ya Ahmadiyya Khalifa Mtukufu wan ne Hadhrat Mirza Tahir Ahmad (rh) tarehe 29/04/1984 alifanikiwa kuhama katika nchi ya Pakistan alikokuwa anatafutwa na maadui wa Ahmadiyya wa Pakistan waliotaka kumwangamiza yeye pamoja na Jumuiyya yake ya AHmadiyya na tarehe 30/04/1984 Khalifatul Masih – IV Hadhrat Mirza Tahir Ahmad (rh) ikawa amefika katika jiji la London Uingereza salama usalimini na ikawa utabiri wa Mwenyezi Mungu umetimia kwamba; "Bila shaka sisi tunawanusuru mitume wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi" (40:52).

Hivi sasa katika ulimwengu wa Kiislam zipo taasisi za Kiislamu ambazo sio wa Ahmadiyya wanaoamini kwamba ni lazima katika dini tukufu ya Kiislam awepo kiongozi (Khalifa) atakayewaongoza Waislam duniani kote kwa mfano taasisi ya Kiislam inayoitwa 'ISLAMIC EDUCATION PANEL' yenye Makao Makuu yake Jijini Dar es salaam imechapisha kitabu chake kinachoitwa 'Kuhuisha na kusimamisha Uislam katika Jamii' (Uk. 16 – 17) wa kitabu hicho wamesema kwamba; "Nyenzo kuu inayomuwezesha mwanadamu kuwa Khalifa ni Elimu ya mazingira aliyotunukiwa na Mola wake na elimu ya mwongozo aliyoshushiwa kutoka kwake Mwenyezi Mungu …… Uk.17 Khalifa, ni kiongozi anayeongoza kwa niaba ya Allah (SW) hapa ulimwenguni, yaani yule anayesimamisha ufalme wa Allah (SW) …….. pamoja na mwanadamu kukusudiwa kuwa Khalifa katika ardhi, si kila mtu atakuwa Khalifa. Ahadi ya Ukhalifa imetolewa kwa watu maalum kama tunavyojifunza katika Kurani Tukufu sura ya 24:56.

Sawa na maelezo hayo ya hapo juu inaonesha wazi kabisa kuwa dawa pekee ya Waislam na wanadamu wote kwa jumla wakitaka kupata ustawi wa maisha yao ya kiroho na ya kidunia ni lazima waungane na Jumuiyya na wawe chini ya nidhamu ya kiongozi mmoja duniani kote anayeitwa Khalifa aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu mwenyewe. Kwa maana hiyo hivi sasa la mgambo la Mwenyezi Mungu limelia kutoka mbinguni.

Ndugu zanguni Waislam pamoja na wanadamu wote njooni kwenye Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya ambayo ni Jumuiyya pekee ya Kiislam duniani kote ilivyokuwa na kiongozi mmoja wa kidunia yaani Khalifa Mtukufu ambapo kutokana na uongozi wake Islam hivi sasa inapata nguvu na maendeleo makubwa sana duniani kote. Lakini mkikataa neema hii ya Ukhalifa basi kama Alivyosema Mwenyezi Mungu katika Kurani Tukufu kwamba ……. "Na watakaokufuru baada ya hayo basi hao ndio wavunjao amri" (24:56) kama nilivyoanza kueleza mwanzoni mwa makala yangu kuwa taasisi ya Biblia ni jibu imewapotosha watu wengi wakinukuu aya za Kurani Tukufu pamoja na Hadithi wanazosema kwamba eti hizo hadithi ni maelezo ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ukweli ni kwamba watu hawa Biblia ni JIbu hawana elimu yoyote ya kufahamu mafundisho ya dini ya Kiislamu na ni naamini hata hiyo dini yao ya Ukristo wanayosema ameianzisha Yesu hawaielewi vizuri. Kwanza ifahamike kuwa aliyeteremshiwa maneno ya Kurani na Hadithi ni mtu mmoja tu, yaani ni Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwa mantiki hiyo maneno ya Kurani Tukufu na Hadithi za Mtume (saw) haviwezi kutofautiana maelezo yake. Na ndio maana Mwenyezi Mungu Anasema katika Kurani Tukufu kwamba, "Enyi mlioamini, mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka kati yenu, na kama mkigombana juu ya jambo lolote, basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho …" (4:60) kwa hivyo basi Hadithi yoyote itakayoeleza kinyume nya Kurani Tukufu Hadithi ni ya uongo sio maneno ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw), tena Mwenyezi Mungu Amesema katika Kurani Tukufu kwamba, "Hizo ndizo ishara za Mwenyezi Mungu Tunazokusomea kwa ukweli, basi hadithi gani watakayoamini baada ya Mwenyezi Mungu na Aya zake?" (45:7) aya hiyo hapo juu inaeleza kwa uwazi kuwa Hadithi zinazotakiwa kuaminiwa ni zile tu zisizokwenda kinyume na maneno ya Kurani Tukufu ni kweli kuwa watu wengi walitunga hadithi nyingi za uongo wakasema zimesimuliwa na Mtume (saw) kumbe sio kweli na hata kama hadithi iwe katika kitabu gani mashuhuri cha Kiislamu inatakiwa kukubaliwa kwa sharti hadithi hiyo haipingani na maagizo na maneno matakatifu ya Mwenyezi Mungu yaliyomo katika Kurani Tukufu.

Ndugu wasomaji wapendwa waandishi wa Biblia ni Jibu katika machapisho yao mbalimbali wamenukuu aya mbalimbali za Kurani Tukufu na Hadithi walizosema eti ni masimulizi ya Mtume (saw) kwa mfano wamenukuu aya ifuatayo kwamba; "Enyi mlioamini ingieni nyote katika utii, wala msifuate nyayo za shetani, bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri" (2:209). Lakini kutokana na chuki, husuda na hiyana waliyokuwa nayo kwa makusudi wamethubutu kupotosha tafsiri ya maneno ya Mwenyezi Mungu ya Kurani Tukufu kwa kunukuu kama ifuatavyo; "Enyi mlioamini ingieni katika hukumu za Uislamu zote" (2:208).

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Utume unaendelea

Kutoka uk. 12

tunavyowabainishia aya, kisha tazama wanageuzwa wapi?

Sasa ndugu yangu Salehe hebu ieleze hiyo aya na ujaribu kukokotoa kama wasemavyo wanahesabati na kupata ndanimwe uhai wa Nabii Isa na iwe ya kwamba sisi tunaosema amefariki tangu zamani ndio tunaoshangawa na Mwenyezi Mungu, Subhana Wataallah.

Jambo jema kati yangu nawe ni kwamba sote tunaamini ujio wa Isa bin Marim katika zama za mwisho. Sasa ikiwa yule nimngojeae mie si yule wa wana wa Israel maana alikwisha kufa, basi ni yupi huyo Isa bin Mariam mwingine ajae? Na kuna ushahidi gani ndani ya Kurani Tukufu juu ya kufika kwake?

Naam, Kurani Tukufu haikuacha jambo na hasa kuhusiana na matukio muhimu katika imani kama hili.

Atakaekuja ni kwa mfano wa yule wa wana wa Israel , rejea aya ifuatayo:-

43:58:- Na anapotajwa mwana wa Mariam kwa namna ya mfano ndipo watu wako wanaupigia kelele.

43:59:-Na husema: Je miungu yetu ni bora au yeye? Hawakuelezi hayo ila kwa kujadiriana tu; bali hao ni watu wagombanao.

Unajua Salehe, Waislam wanakuja kuwa na miungu kwa namna gani? Sasa ngoja nikueleze wakati mimi nakueleza kutoka kitabu cha Mwenyezi Mungu ya kuwa Kurani inasema kuwa Yesu kafa. Wengi katika Waislam maamuma au hata baadhi ya Mashekhe, atakwambia lakini mbona Sheikh fulani kasema hivi au anasema hivi. Kwa maana hiyo basi hao mashehe fulani kasema hivi ndiyo miungu watakayokuwa nao Waislam kama wakina Didas, wakina Rashid Said Ally wa Alfujaira n.k. Hata sasa bwana Salehe nahisi akili yako inapepesukia huko maana kutoka kwa Subhana Wataallah kupita kitabu chake huna kitu, kitabu ambacho kinakwambia huyo Ibni Maryam anaekuja ni wa mithili wa yule wa wana wa Israel na si mwenyewe halisi. Na kitabu chake alichoshuka nacho ni Kurani Tukufu hii hii kama nilivyokwisha kukueleza katika makala ya pili (Sura Albaqara).

Kumbuka kelele tunazopiga watu wake Muhammad s.a.w. zinaonyesha kumwuzi Mwenyezi Mungu lakini anatusamehe na kutuachia Ukhalifa licha ya pengine angeweza kutotupa kwa ushupavu tunaouonyesha .

43:61:- Na kama tungelipenda tungewafanya malaika kuwa Makhalifa katika ardhi badala yenu.

Tunashukuru Ukhalifa huu wa Ahmadiyya unaendelea kutokana na Mwenyezi Mungu kutoamua vinginevyo na kwa kuwa wapo na walikuwepo walioamini na wanaendela kujitokeza kwa malaki kila mwaka wanaojiunga na ukhalifa huu wa masihi wa Muhamad Isa bin Maryam wa mfano. Salehe Wallahi acha kuangalia kwa macho yako hayo tuyaonayo, angalia kwa macho ya kiroho pia tafadhali bwana.

Kuzidi kukithibitishia kifo cha Nabii Isa naona niongeze aya moja katika mbili.

16:21:- Na wale ambao wanawaita badala ya Mwenyezi Mungu hawaumbi chochote bali wao wameumbwa.

16:22:- Ni wafu si wazima na hawajui watafufuliwa lini.

Nabii Isa a.s. anaabudiwa kama nafsi ya pili ya mungu au mungu mwenyewe. Hivyo zama inashuka aya hii lazima nae atakuwa alikwisha kuwa katika hali ya umauti. Watu wengi ambao huwa tunajadiriana nao mada hizi wakifikishwa hapa hukimbilia kun faya kun bila kuelewa kuwa kun faya kun siku zote haiwezi kuvunja kawaida zake Mwenyezi Mungu pia.

Kun faya kun haiwezi kumwingiza Mwenyezi Mungu katika kusema uongo, kufanya hiyana, kuoa na kuzaa, Vyote hivyo ni mbali kabisa na Utukufu Wake Subhana Wataallah,

Kwa hiyo ndugu yangu haiwezekani Mwenyezi Mungu Atuambie wale waliokuwa wakiabudiwa kama miungu wakati inashuka aya hii ni wafu halafu awepo mmoja mzima na huyo mmoja ndiye maarufu zaidi kuliko wote wanaoabudiwa kama miungu je Salehe unapimaje hili?

Katika sura hii kuna aya nyingine inayothibitisha kifo cha Nabii Isa pale ambapo siku ya kusimama hesabu atakapoulizwa juu ya kuabudiwa kwake yeye na mama yake na kuonyesha kwamba hana habari kabisa na jambo hilo

Kama ingewezekana arudi duniani si angekuwa ameliona hilo? Na asingekana siku ya kusimama hesabu kuwa na habari hiyo na swali lingeulizwa kwa namna nyingine ikitajwa awamu yake ya kwanza kuwepo duniani kabla ya kurufaishwa kama uaminivyo wewe.

Naomba niishie hapa kutoka sura hii kuhusu kuendelea kwa Utume wa kurudisha watu kwenye njia iliyonyooka huku nikihadharisha ya kwamba kwa Kurani hii Mwenyezi Mungu Humwongoza mwenye kutafuta radhi yake katika njia ya salama na Huwatoa watu katika giza kuwapeleka kwenye nuru kwa amri Yake, na kuwaongoza kwenye njia iliyonyooka.

Tuweni basi wenye kutafuta radhi Yake kwa kuitafuta haki na mwongozo ili tupate kuongozwa

Amin.

Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya

Kutoka uk. 12

yake katika kuhubiri Uislam Afrika Mashariki.

Barua aliyomuandikia Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Sheikh Mubarak Ahmad ni barua inayoonesha heshima na shukrani kubwa kwa Mwalimu wake na masikitiko yake makubwa ya kutoweza kuonana. Mvuto huu wa Sheikh Mubarak Ahmad ni mvuto unaotokana na ukweli ya kwamba alilipenda sana Taifa hili. Mimi aliwahi kunieleza ya kwamba katika sala zake zote hakumbuki ya kwamba kuna wakati aliposahau kuiombea Tanzania na viongozi wake. Na alinieleza pia ya kwamba kila alipomuandikia Khalifa Mtukufu wa Pili (ra) alimuomb katika barua hiyo aiombee nchi ya Tanzania. Baadhi yetu tunaweza kuelewa sasa kiini na msingi wa amani na upendo vitu ambavyo havipatikani mahali popote katika Afrika isipokuwa Tanzania. Bila shaka huu sio ujanja wetu bali ni fadhila kubwa ambayo ilituangukia kuwa na kiongozi aliyeipenda sana nchi hii na kuwapenda watu wake.

Mwalimu Omari Mnungu anaeleza ya kwamba alipokwenda katika mkutano wetu mkuu huko London mkutano wa mwaka, wajumbe wote wa Tanzania mara alipokwishawaona Sheikh Mubarak hakutaka kabisa kuachana nao. Huku machozi yakimtoka aliwakusanya wote kwa mapenzi makubwa kama vile mama kuku anavyowahifadhi vifaranga wake. Na kila aliyemuuliza hawaninanimbonahuondokani nao? Yeye alisema hawa ni watoto wangu. Ninakumbuka pia ya kwamba alipokuja katika safari hiyo ya kutayarisha safari ya Khalifa Mtukufu wa nne (rh) kila aliyemuona alikumbatiana naye na kwa kutumia mkia wa kilemba chake aliendelea kufuta machozi. Jambo la kufurahisha sana ni kwamba alipofika uwanja wa ndege kijana mmoja alimuuliza kwa kiingereza 'Mzee Passport yako ipo wapi?' kwa kutabasamu alimueleza kwa Kiswahili; 'Mwanangu unaniuliza mimi passport niliyekuwa hapa toka mwaka 1934 na hata Julius Kambarage Nyerere hawezi kuniuliza Passport'. Huo ndio ulikuwa ukaribu wa Sheikh Mubarak Ahmad na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere sehemu muhimu sana katika historia ya ukombozi wa nchi hii. Na kama tulivyojenga hoja, mwandishi yeyote wa historia ya maisha ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere hawezi kuwa amekamilisha kazi yake kama hakuona nafasi ya Ahmadiyya na Waahmadiyya katika maisha ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.



Mzee Suleiman Tofiq (katikati) akisalimiana na Dr. Abdul Salaam (Muislamu wa kwanza kutunzwa tuzo ya Nobel ya Fizikia) ambaye alitembelea hapa nchini kwa mwaliko wa Mwl. Julius Nyerere. Katikati yao (mwenye kofia ya Jinah Cap) ni Sheikh Malik.

Mwalimu Nyerere na Mzee Suleiman Tofiq

Kati ya mwisho wa vita ya ukombozi 1907 hadi kuasisiwa jeshi jingine la ukombozi Tanganyika African National Union mwaka 1954, hapo kati kati Watanganyika walikwishateswa kiasi cha kutosha, walishaona mengi, kujifunza mengi na uzoefu huo uliwapambanulia ya kwamba ili kuondoa dhuluma na mateso umoja unatakiwa na umoja unapatikana kwa vikundi vya kutetea maslahi yao. Katika kipindi hicho vikundi vifuatavyo vilianzishwa tukivitaja vichache; *Tanganyika Territory Civil Service Association*, Chama cha Makuli, *African Dockworkers Union* (1937), Wapishi na Madobi, *Association of cooks washer men* (1939) Wapishi na watumishi wa ndani (*Association of cooks and domestic servants* (1939), Madereva (*African Drivers Association* (1944) moja ya kikundi ambacho juu ya udogo wake mbegu ya *Tanganyika African National Union* (TANU) iliweza kuota hadi ikatuletea taifa jipya la Tanganyika, kikundi hicho ni *Tanganyika African Association* (TAA).

Kabla hatujakitazama kwa jicho la ndani, kikubwa hatuna budi kueleza mazingira yaliyosaidia kwa kiwango kukuwa *Tanganyika African Association*. Katika hili tungependa kusisitiza jambo moja wakati umefika wa wanahistoria wetu kutawaliwanauadilifu.Uadilifu ni nini? Uadilifu ni jitihada za kutumia mizani bila ya jicho la husuda. Chembechembe za husuda hupoteza kabisa mguso wa uadilifu. Mtu kwa sababu hatawaliwi na adili hudiriki kuita juwa mwezi!. Tutizame jambo lilivyo na kuogopa kusutwa dhamira, tuseme kweli kama tunavyoiona. Huo ndio uadilifu ambao kwa bahati mbaya wanahistoria wengi hawana. Kabla hatujaangalia umuhimu wa kutumia jicho la uadilifu tutizame maisha ya Madiba Mandela.

Mandela alikuwa mpinzani mkubwa wa ubaguzi wa rangi na kwa harakati za kuleta mabadiliko katika Afrika Kusini akatiwa ndani miaka 27. Jicho la uadilifu nani kiongozi wa Afrika angemvumilia Mandela hata kwa sekunde moja? Je hatuna msululu wa viongozi wa Afrika waliouawa kwa kuwa na mawazo tofauti na walioko madarakani? Tutaje mifano michache Diallo Terli Katibu wa kwanza wa O.A.U uliza watu wa Guinea yaliyomkuta, Patirice Lumumba aliuawa kikatili huwezi kutenganisha mauaji hayo na Joseph Kasaruba na Moise Tshombe, Tom Mboya aliawa mchana kweupe na jina kubwa lililohusika likafunikwa. Wengine ukikosana nao tu si matusi na kudhalilisha kama yaliyofanyika kwa Kassim Hanga. Hoja yangu ni kwamba Fredrick de Klerk ameonesha utu zaidi kuliko viongozi wengi wa Afrika. Isingechukua sekunde, kummaliza Mandela. Kuheshimu na kutambua tendo hili la kutomaliza maisha ya Mandela ndilo hasa kiini cha uadilifu katika historia.

Mwezi April 1925 Sir Donald Cameroon alikuwa Gavana wa pili wa Tanganyika baada ya kuondoka kwa Gavana wa kwanza Sir Horace Byatt aliyeanza kazi yake tarehe 22 Julai 1920. Sir Donald Cameroon kabla ya kuwasili nchini alikuwa Nigeria chini ya Lord Jiugard mwanzilishi wa sera ya kuwatawala Waafrika kwa kutumia taasisi zao za jadi zilizo kuwepo kabla ya uvamizi wa wakoloni. Kilichowaleta ni unyonyaji wa rasilimali zetu. Cameroon ni mtu aliyepanda ngazi za madaraka kutoka chini hadi juu kwa kutumia juhudi na maarifa. Katu hakutegemea vyeti ambavyo hata hivyo hakuwa navyo. Historia hii ilimsaidia kuheshimu bidii za mtu. Kukaa ofisini amezungukwa na karatasi haikuwa khulka yake. Alipenda kwenda nje ya ofisi kuona kwa jicho lake na kujifunza. Toka ujana wake aliwahurumia sana watu wa chini waliyo onewa. Na sururi yake daima ilikuwa ni kuhakikisha wanaoonewa wakipewa haki yao.

Siku mbili tu akiwa nchini alisema; "Tuko hapa kwa niaba ya baraza la udhamini (League of Nations) kuwafundisha Waafrika viwango vinavyotakiwa. Wakishafikia hapo tutafunga virago, kwani hatutakuwa na lolote jingine la kufanya. Itachukua muda, lakini kila tunachokifanya kisimamie kwenye msingi huo".

Sir Donald Cameroon aliheshimu sana aliyoyasema na kuahidi. Walowezi kutoka Kenya walikuja kwake kuomba ardhi katika nyanda za juu kusini. Jibu alilowapa liliwaacha hoi na vinywa wazi. Labda hili ni somo kwa wale wanaochezea ardhi yetu kwa hivi leo. Aliwauliza walowezi; "Mmekwisha tuma maombi kwa DC huko Iringa ambaye naye atayawakilisha kwa tawala za wenyeji ambao katika nchi hii ndio wanaoamua nani apate au asipate ardhi. Hata Lord Delamere yule kabaila mkubwa wa Kenya hakuambulia lau punje mkononi, aliondoka mikono mitupu"!

Kama tulivyokwishagusia, Cameroon hakuamini utamaduni wa kukaa ofisini na kuagiza mafaili. Yeye alitoka na kwenda kuona mambo yalivyo kuwa yakitendeka. Alipenda kuona Waafrika wakiendesha mambo yao kwa kujiamini. Alishirikiana na wale machifu waliokubalika na walichapa kazi. Na alipenda kuwatembelea watu na kuzungumza nao. Akiwa Mwanza aliuambia umati uliokusanyika kwamba katika miaka mitatu alikuwa amejenga barabara na alikuwa amewatuma mabwanashamba watoe elimu ya kilimo. Kwa hiyo akasema ni wakati wa Watanganyika walime pamba zaidi, Kambarage mmoja wa wasikilizaji aliamsha mkono, Sir Donald Cameroon akamruhusu azungumze, "Umefanya yote uliyoyasema, sasa tunachotaka utuletee mvua ya uhuru kwa raia. Itakumbukwa pia wala hakumuweka ndani. Sijui viongozi wangapi katika Afrika wangevumilia hilo.

Kwa ujumla Sir Donald Cameroon alipenda kusikia maoni ya watu wengine na upo ushahidi. Kwa kiwango Fulani alitoa ushirikiano kuhusu sheria ya kuanzishwa kwa Tanganyika African Association (TAA). Mtu mwingine aliyeongeza hamasa katika kuanzishwa kwa Tanganyika African Association ni msomi maarufu wa Ghana. Dr. James Kwegyur Aggrey.
Dr. Dr. James Kwegyur Aggrey alizaliwa katika nchi iliyokuwa inaitwa Gold Coast sasa Ghana mwaka 1875. Alipata elimu yake shule ya Methodist, chuo cha Livingstone na baadae kupata shahada ya uzamili katika chuo kikuu cha Columbia Marekani.

Katikati ya mwaka 1920 – 1924 alikuwa mjumbe wa tume ya Phelps – Sookes ambayo ilitumwa kuchunguza elimu ya Waafrika. Wakati akitumikia kamati alizuru Tanganyika. Mjumbe huyu hakuruhusiwa kulala New African Hotel kwa sababu ya rangi yake. Kutokana na tukio hili Sir Donald Cameroon alimpatia nafasi katika nyumba ya serikali. Vugu vugu hili la Dr. Aggrey kubaguliwa na msaada wa Sir Donard Cameroon mwaka 1929 kilizaliwa African Association (AA) kikiwa na viongozi wafuatao; Kleisi Sykes – Katibu wa kwanza, Mzee bini Sudi, Ibrahim Hamisi, Raikes Kusi, Rawson Watts – Rais wa kwanza, Ali Saidi Mposi – muweka hazina, Zibe Kidasi, Suleiman Majidi, Cecil Wadde na Erikh Fiab.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Rabiul I/Rabiul II 1435 AH | February 2014 | Tabligh 1393 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Said r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Mfanya biashara mkweli mwaminifu ndiyo pamoja na manabii na masiddiki na mashahidi. (*Sunan Darmi, Tirmidh*)

Utume kuwarudisha watu kwenye njia iliyonyooka unaendelea

Eng. K. S. Kazema
MOROGORO.

Assalam Aleikum ndugu msomaji wa makala hizi ambazo namjibu ndugu, rafiki yangu bwana Salehe Abdul wa hapa Morogoro juu ya ujumbe wa mahubiri aliouacha ofisini kwangu uliosimamia kwamba hakuna tena Utume baada ya Mtume wetu mtukufu Seidina Muhamadi Mustafaa s.a.w.

Sasa basi naendelea kuelezea juu ya kuendelea utume kutoka Sura hii hii ya tano na leo nampa aya ya pili na kama nafasi itaruhusu na ya tatu pia kutoka sura hii ya tano

Bismillah –Rahmanir Rahiim

SURA IMRANI.

Kwanza kwa mara nyingine niseme Alhamdulillah Rabil-laalaamin kwa Mwenyezi Mungu kunipa afya na fulsa nyingine kuendeleza mjadala huu kama nilivyoahidi huko nyuma kuendeleza hoja hii kutoka Sura moja hadi nyingine katika Kurani tukufu nikimjibu bwana Salehe Abdu wa Morogoro.

Naamini hoja nilizotoa kujibu hoja yako ya kutumia aya ***5:20*** kufungia Utume umeipata na sidhani kama una hoja dhidi ya hoja nilizotoa ambapo leo naongeza aya nyingine.

Lau aya ambayo pia naiweka mbele yako ni Mutashyabiat lakini inapounganishwa na imani yako juu ya Utume kutoendelea inakuwa kama kichocheo cha kukazia kuendelea Utume usio na sheria duniani na inatengua kijiwe ulichosimamia na unaporomoka umekosa pa kujishikiza ndugu.

Umeandika katika majibu yako kwamba Nabii Isa ni alama ya kiyama na pindi atakapodhihiri basi kiyama kimefika. Kwa maana hiyo imani yako ni kwamba Nabii Isa yu hai mbinguni na iko siku atashuka!!!!

Ajabu katika biblia ipo aya ikimnukuu Nabii Isa akisema:-

Hakuna atakaepaa mbinguni ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni.

Sasa tazama ikiwa kushuka kwake kutoka mbinguni kulikuwa kupitia njia za kawaida



Eng. K. S. Kazema
Mwandishi wa makala hii

kwa kuzaliwa kwa uchungu na kukua toka utotoni mpaka utu uzima hakuna shaka kupaa kwake mbinguni kutakuwa kwa njia za kawaida, kupita umauti. Bahati nzuri kurani pia inaunga mkono njia hiyo pale Mwenyezi Mungu anaposema:-

3:56 (Kumbukeni) Mwenyezi Mungu aliposema: Ewe Isa, kwa yakini mimi nitakufisha na nitakuinua kwangu ……..

Kwa hiyo kufa kunatangulia kisha roho inainuliwa kwake Rahmani.

Lakini Yesu anatabiri kwa waliokuwepo kwamba watakuwepo watakaompaza (wakina Salehe) bila kutazama au kutilia maanani alishuka vipi.

Tazama Nabii Isa anavyotaka kuwafikirisha ndugu zangu hao lakini wapi hawaoni wamekazana, lilitumika neno kupaa basi kinyume chake ni kushuka tu hivyo lazima iko siku atashuka tu! Pole sana bwana Salehe nakushangaa.

Lakini mshangao mkubwa zaidi unatoka kwa yeye Mwenyewe Subhana Wataallah katika aya ambayo ndiyo ya pili kutoka sura hii kusaidia hoja ya kuendelea Utume maana huyo wanaemngoja wale 72 hatakuja tena. Kwanza :

1. Kawaida za Mwenyezi Mungu hazibadiliki ***33:63, 17:78 etc***
2. Nabii Isa bin Mariam ni binadamu hakupewa mwili usiokula chakula ***21:9***
3. Kwa kuwa sasa hali chakula basi kama marehemu wengine hawali chakula akiwemo mtukufu mama yake kwa hiyo na yeye pia yumo katika hali aliyomo mama yake.
4. Mwenye kupewa umri mrefu hupindishwa katika umbo na kurudishwa katika hali dhalili. Kama angekuwa hai umri wa miaka 2000 angekwisha sagika kabisa n.k.

Hivyo kwa ujumla Nabii Isa alikwisha kufa na Mwenyezi Mungu anawashangaeni katika aya hii; Wakristo na Waislam kundi la wale 72.

5:76:- Masihi bin Mariam siye ila ni Mtume tu; bila shaka Mitume wamekwishafariki kabla yake; na mama yake ni mwanamke mkweli, wote wawili walikuwa wanakula chakula. Tazama jinsi

Endelea uk. 10

Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya

Na Mahmood Hamsin
Mubiru - Dar es salaam

Kutoka Toleo lililopita

Mwaka 1961 nchi ya Tanganyika ilipopata uhuru, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa bado anamkumbuka Sheikh Mubarak Ahmad na wakati bendera ya Tanganyika inapandishwa na ile ya Union Jack inateremshwa Sheikh Mubarak Ahmad alikuwa uwanjani akiwakilisha Islam katika maombi ya kuiona bendera ya Tanganyika ikipandishwa. Bila shaka heshima hii inatokana na mchango mkubwa ambao unaonekana kusahaulika wa mwanachuoni huyu wa Kiislam. Historia ya Kenya pia ukiitazama kwa undani utauona urafiki aliokuwa nao Sheikh Mubarak Ahmad pamoja na Jomo Kenyata. Na ndiye Sheikh huyu aliyemwendea Jomo Kenyata gerezani na kumkabidhi tafsiri ya Qur'an Tukufu katika Kiswahili na kumuombea ya kwamba Mwenyezi Mungu akipenda atatoka gerezani. Na hivi ndivyo ilivyokuwa.



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akipokea Tafsiri ya Qur'ani tukufu kwa Kiswahili pamoja na vitabu vingine vya dini ya Kiislamu kutoka kwa Sheikh Waseem Ahmad Cheema aliyewahi kuwa Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania.

Tarehe 09 mwezi wa Disemba 1961 katika viwanja vya Ikulu palifanyika sherehe ya kukata na shoka ya kushangilia uhuru wa Tanganyika. Sheikh Mubarak Ahmad alikuwa miongoni mwa watu maarufu waliopewa mwaliko maalum wa kuhudhuria tafrija hiyo. Na mwaliko huo ikumbukwe ulikuwa unatoka kwa waziri Mkuu wa Tanganyika Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Pamoja na Sheikh Mubarak alikuwepo Sheikh Kaluta Amri Abedi na Maulana Sheikh Muhammad Munawwar. Kwa furaha na bashasha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipita katika bustani ile ya Ikulu akiwasalimu wote wageni wake na alipofika walipokuwa Sheikh Mubarak Ahmad, Sheikh Muhammad Munawwar na Sheikh Kaluta Amri Abedi kwa haraka alimwambia yule mhudumu wake ya kwamba tafadhali ondoa haraka pombe mahala hapa, kwa sababu hawa ni Masheikh na hawa hawatumii pombe. Akawaomba sana radhi na wakatengewa mahala mbali kidogo mahala ambapo hapana pombe. Huo ni ushahidi mwingine tosha unaonesha jinsi gani kiongozi wa kwanza wa Tanganyika alivyoielewa vizuri Jumuiyya ya Ahmadiyya na kuheshimu yote waliyokuwa wanayaheshimu.

Sheikh Mubarak Ahmad alipokuja tena mwaka Tanzania mwaka 1988 katika matayarisho ya safari ya Khalifa Mtukufu wa nne Hadhrat Mirza Tahir Ahmad (rh) hakuweza kufanikiwa kukutana na Mwalimu Nyerere, lakini aliweza kufika nyumbani kwake na akaweza kumkabidhi mama Maria Nyerere ambaye walikuwa wanajuana kwa miaka mingi, zawadi za vitabu kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Katika vitabu hivyo kimoja wapo kilikuwa ni cha 'My mother' ambacho kimeandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan ambaye alikuwa rafiki mkubwa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kama tutakavyoona baadae. Barua ya kupokea vitabu hivyo na kuonesha masikitiko ya kutoweza kuonana nae iliandikwa na mwanafunzi kwa Mwalimu wake, na hii inapatikana katika kitabu cha Sheikh Mubarak Ahmad kinachohusu maisha

Endelea uk. 11